

NATIONAL ASSEMBLY

OFFICIAL REPORT

Wednesday, 14th March 2018

The House met at 9.30 a.m.

*[The Temporary Deputy Speaker
(Hon. (Ms.) Mbalu) in the Chair]*

PRAYERS

QUORUM

The Temporary Deputy Speaker (Hon. (Ms.) Mbalu): Order, Hon. Members! For us to have the requisite quorum, I order that the Quorum Bell be rung.

(Quorum Bell was rung)

Order, Members! I can now confirm that we have the numbers for us to start business.

PAPERS LAID

Hon. Washiali: Hon. Temporary Deputy Speaker, I beg to lay the following Papers on the Table of the House:

The Sacco Societies Deposit Levy (Amendment) Order, 2018 and the Explanatory Memorandum.

The Political Parties (Registration) Regulations, 2017 and the Explanatory Memorandum.

The Political Parties (Funding) Regulations, 2017 and the Explanatory Memorandum.

The Political Parties (Political Parties Liaison Committee) Regulations, 2017 and the Explanatory Memorandum.

The Reports of the Auditor-General on the Financial Statements in respect of the following Constituencies for the year ended 30th June, 2016 and the certificates therein:

(a) Nyaribari Masaba Constituency.

(b) Wajir South Constituency.

(c) Awendo Constituency.

(d) Nyaribari Chache Constituency.

(e) Tarbaj Constituency.

(f) Wajir East Constituency.

(g) Nyatike Constituency.

(h) Muhoroni Constituency.

(i) Bobasi Constituency.

(j) Suna East Constituency.

(k) Kuria East Constituency.

- (l) Bonchari Constituency.
- (m) Kabondo Kasipul Constituency.
- (n) Bomachoge Chache Constituency.
- (o) Rangwe Constituency.
- (p) Kitutu Chache South Constituency.
- (q) Kisumu East Constituency.

The Temporary Deputy Speaker (Hon. (Ms.) Mbalu): Let us have the chairman of the Departmental Committee on Transport, Public Works and Housing.

Hon. Losiakou: Hon. Temporary Deputy Speaker, I beg to lay the following Paper on the Table of the House today, Wednesday, 14th March 2018:

The Report of the Departmental Committee on Transport, Public Works and Housing on the consideration of the Nairobi Metropolitan Area Transport Authority Bill 2017.

I thank you, Hon. Temporary Deputy Speaker.

The Temporary Deputy Speaker (Hon. (Ms.) Mbalu): Order, Hon. Members! Order No. 5 is in reference to the Papers by the Leader of the Majority Party presented by Hon. Washiali. On the Sacco Societies Deposit Levy (Amendment) Order, 2018 and the Explanatory Memorandum, pursuant to Section 15 of the Sacco Societies Act, I do refer it to the Committee on Delegated Legislation. With regard to the Political Parties (Registration) Regulations, 2017 and the Explanatory Memorandum; the Political Parties (Funding) Regulations, 2017 and the Explanatory Memorandum; and the Political Parties (Political Parties Liaison Committee) Regulations, 2017 and the Explanatory Memorandum, pursuant to Section 49 of the Political Parties Act 2011, I also refer these to the Committee on Delegated Legislation. The Chairperson and the Members of the Committee, please, take note of this.

NOTICE OF MOTION

The Temporary Deputy Speaker (Hon. (Ms.) Mbalu): We have a Notice of Motion from the Leader of the Minority Party, Hon. Mbadi.

BUILDING BRIDGES TO A NEW KENYAN NATION

Hon. Ng'ongo: Hon. Temporary Deputy Speaker, I beg to give notice of the Following Motion:

THAT, acknowledging that the meeting between His Excellency the President, Hon. Uhuru Kenyatta and the distinguished Leader of the NASA Coalition, His Excellency Hon. Raila Odinga of Friday, 9th March, 2018 put aside political differences through building bridges and marked an important and historic moment for the country; aware that this extraordinary opportunity will enable Kenyans to face and address the challenges currently faced, and openly and honestly discuss successes and failures and finally formulate and implement the necessary corrective measures for the country to move forward; cognisant that, ahead of and immediately after the 2017 General Election, Kenya witnessed a number of political upheavals including and not limited to the demonstrations and hate speech which threatened to polarise the country along political and ethnic differences; recognising that the initiative by the two leaders made on 9th March, 2018 on 'Building Bridges to a new Kenyan Nation' and aimed at ensuring an all-inclusive and cohesive nation will require facilitation and support from all arms of Government and relevant institutions; committed to the determination of all Kenyans to live in peace as one indivisible sovereign nation; further recognising that there is need to roll out and implement

programmes on shared objectives in a bipartisan manner as was agreed by the two distinguished leaders-

NOW THEREFORE-

(a) the thanks of this House be recorded in commending the two distinguished leaders for providing leadership in the patriotic task of promoting unity, peace and harmony in the country and initiating the move towards 'Building Bridges to a new Kenyan Nation'; and

(b) this House commits itself to support and advance, within its mandate, the aims and objectives of the initiative of 'Building Bridges to a new Kenyan Nation'.

The Temporary Deputy Speaker (Hon. (Ms.) Mbalu): Thank you. The Notice of Motion is procedurally done. Next Order!

BILL

First Reading

THE CONSTITUTION OF KENYA (AMENDMENT) (No.2) BILL

(Order for First Reading read - Read the First Time and ordered to be referred to the relevant Departmental Committee)

HOJA

KUANZISHA HOSPITALI YA RUFAA YA KITAIFA KATIKA KAUNTI YA MOMBASA

The Temporary Deputy Speaker (Hon. (Ms.) Mbalu): Ningependa kumwalika Mtoa Hoja, Mbunge wa Nyali, Mhe. Mohamend Ali Mohamed.

Hon. Mohamend Ali: Mhe. Naibu Spika wa Muda, naomba kuwasilisha Hoja ifuatayo:

KWAMBA, tukifahamu Kifungu cha 43 cha Katiba ya Kenya kimeweka wazi kwamba kila Mkenya ana haki ya kuwa na kiwango bora cha afya kinachojumuisha afya bora ya uzazi; aidha, katika utaratibu wa Ajenda ya Maendeleo ya baada ya Mwaka wa 2015, dunia imewajibikia Afya kwa Wote na kutimiza Lengo Endelevu la Maendeleo la tatu (SDG-3) kuhakikisha na kuendeleza maisha na afya bora kwa wote; tukiafiki, uwekezaji katika sekta bora ya afya ni muhimu kuhakikisha kila mtu anapata huduma za kimsingi za afya bila kuzingatia eneo analotoka au hali yake ya kiuchumi; tukitambua, asilimia 80 hutegemea huduma ya afya ya umma ilihali kuna hospitali mbili pekee za rufaa nchini ambazo ni Hospitali ya Kitaifa ya Kenyatta - Nairobi na Hospitali ya Rufaa na Mafunzo ya Moi - Eldoret; tukizingatia, Kifungu cha ishiringi na tano (25) kikiambatanishwa na Mpangilio wa Kwanza wa Sheria ya Afya 2017 kinasema kutakuwa na hospitali ya kitaifa ya rufaa katika kila gatuji (Level 6); Bunge hili linahimiza Serikali kuharakisha kuwepo Hospitali ya Rufaa ya Kitaifa katika Kaunti ya Mombasa ili kufanikisha huduma zote za afya zinazohitajika eneo hilo zitumiazo teknolojia pevu na wataalamu wa hali ya juu pamoja na kutoa mafunzo kwa wahudumu wa afya kabla na baada ya kuhitimu.

Mhe. Naibu Spika wa Muda, hili ni wazo ambalo liliwahi kuletwa na Rais Uhuru Kenyatta Juni mwaka uliopita. Rais alipendekeza kwamba katika kila kaunti, kuwe na hospitali ya rufaa. Ningependa kutoa utaratibu wa mambo fulani ambayo yanachangia kuwepo kwa hospitali hizi kwa sababu asilimia 80 ya Wakenya ni wale ambao hawawezi kufikia huduma hizi za afya. Nitaanza kwa kutoa mifano ambayo imesalia katika historia ya Kenya. Nitaanza na kwangu nyumbani kule Mombasa. Kuna mtoto mdogo kwa jina la Satrin Osinya au Baby Osinya aliyepigwa risasi na akakaa na risasi kichwani kwa takriban siku nne kabla ya kuletwa Nairobi ili afanyiwe upasuaji. Hii inamaanisha nini? Inamaanisha kwamba iwapo hatutakuwa na huduma za afya katika kila kaunti, basi tutakuwa katika hali mbaya sana.

Hospitali ya Coast General iliyoko Mombasa inahudumia kaunti sita ambazo zinajumuisha Taita Taveta, Tana River, Kwale na Kilifi. Hizi ni baadhi ya kaunti ambazo zinategemea hospitali hii katika huduma za rufaa. Shirika la Afya Duniani (WHO) lina mapendekezo yake ambayo yanasema kwamba daktari mmoja anafaa ahudumie wagonjwa elfu moja lakini hapa nchini Kenya, daktari mmoja anahudumia wagonjwa elfu kumi. Hili ni jambo ambalo haliwezekani, si la msingi na haliingii akilini. Tangu tupate Uhuru miaka 55 iliyopita, tuna hospitali mbili peke yake ambazo ni hospitali ya kitaifa ya Kenyatta na ile ya rufaa ya Eldoret.

Leo napendekeza na kusema kwamba kila kaunti ipewe hospitali yake ya rufaa ili mwananchi wa kawaida aweze kufikiwa. Si kusema tu zijengwe bali pia nasema zile zilizopo hapo zinaweza boreshwa zaidi na kuwekwa katika kiwango cha Level 6 ambayo itaweza hudumia mwananchi wa kawaida aliye na matatizo chungu nzima. Hospitali ambazo ningelipenda zianze kufanyiwa ukarabarati wa hali ya juu na kuanza kufikia wananchi kufika ile kiwango ya Level 6 ni Meru, Embu, Mombasa, Kakamega, Busia, Jaramogi, Garissa na Kisii ambazo ni Level 5.

Mhe. Spika wa Muda, nadhani utashangaa nikikwambia ya kwamba taifa hili lina madaktari wa kutibu saratani yani *oncologists*, kwa lugha ya kimombo wanaohudumia Wakenya takriban 45 milioni madaktari 23 peke yake. Hawa madaktari ni wa kibinafsi. Namaanisha nini? Wanahudumu katika hospitali ambazo ni za wale ambao wana nguvu kama Aga Khan University Hospital na Nairobi Hospital. Mkenya wa kawaida hawezi kuenda kutibiwa ugonjwa wa saratani katika hospitali hizo. Miaka 55 imepita tangu Kenya ipate Uhuru na tunajipiga kifua tukisema tumeendelea, na ilhali tuna madaktari wa upasuaji yaani *neurosurgeon* 18. Hii ni aibu iwapo tuna madaktari 18 Kenya nzima. Leo tunajipiga kifua na kusema ya kwamba tuna madaktari tosha ambao ni wa figo, kwa lugha ya kimombo tunawaita *nephrologists*. Hawa ni 16 peke yake. Mombasa tuna wawili pekee. Ni nani atawafikia hawa maskini?

Leo Mbunge katika Bunge hili akisikia anasokotwa na tumbo kidogo tu, yeye ana daktari wake wa kipekee. Yeye ana nguvu za kwenda katika hospitali na kuhudumiwa mara ya kwanza. Kule mashinani, kuna watu ambao tumbo zao zinanguruma kama mitambo ya kuchapia mahindi lakini hawajui wataenda wapi, kwa sababu hawana daktari wa kibinafsi, hospitali haziko karibu na iliyoko karibu iko katika kaunti nyingine. Haya ndiyo mambo ambayo nataka tuangalie. Kwa mfano, Kenya nzima madaktari waliosomea taaluma mbalimbali ambazo nimezitaja kama vile saratani, upasuaji na figo ni 425. Nitakupatia utaratibu tu wa kukuonyesha athari ambazo zinaweza kutupata iwapo hatutaweza kushughulikia janga hili, na kupitisha Hoja hii na kuhakikisha kwamba hospitali zimeweza kufika katika kaunti. Nitakupa mfano wa kaunti ya Mombasa ambayo idadi yake ni watu 939,370. Madaktari wanaohudumia watu hawa takriban milioni moja ni 198.

Katika kaunti ya Kwale, watu 649,331 wanahudumiwa na madaktari 65. Hawa ni watu takriban 700,000. Sehemu kama Nyeri ambayo ina watu takriban 700,000 wanahudumiwa na madaktari 143. Kiambu ambayo ina watu takriban 1.6 milioni wanahudumiwa na madaktari 278. Kisumu ambayo idadi yake inakaribia milioni moja, wanahudumiwa na madaktari 163. Ukiangalia kaunti ya Kisii ambao ina idadi ya 1.2 milioni wana madaktari 163, utaona ya kwamba wanahitaji madaktari 989 zaidi. Kisumu wanahitaji madaktari 800. Kiambu wanahitaji madaktari 1,343. Hizi tu ni baadhi ya sehemu ambazo zinaathiriwa sana. Hii ndiyo sababu ambayo imetuleta katika Bunge hili. Tulienda kupiga kampeini na tukawaahidi wananchi ya kwamba tutakuwa sauti yao katika Bunge hili. Tulitoa ahadi zote. Nadhani ahadi ambayo tutaitoa kwa Wakenya na ambayo itasalia miyoni mwao ni ya kuhakikisha katika kila kaunti katika taifa hili kuna hospitali ya rufaa na mwananchi wa kawaida ataweza kuhudumiwa.

Madaktari waliosajiliwa na Serikali na ambao wanajulikana Kenya nzima ni 11,000. Hawa wanahudumia Wakenya 45 milioni. Kati ya hawa madaktari 11,000, wanaofanya kazi, *practising* kwa lugha ya kimombo, ni 6,000 peke yake. Hivi sasa tunapozungumza, kuna wale ambao ni watahiniwa, tunawaita *interns* kwa lugha ya kimombo, ni 1,000. Wakimaliza kusoma, hawana mahala pa kuenda. Watajiunga na wenzao 1200 ambao hawana kazi na wako nje. Kwa ufupi, nasema taifa hili linahitaji madaktari 34,445.

Nitaendelea bado kwa kueleza ni kwa nini hasa tunataka hizi hospitali ziweze kuhudumia wananchi. Nitaanza na masuala ya rufaa. Leo mgonjwa akiwa Nyeri, Kiambu, Mombasa ama Turkana, ataenda katika hospitali iliyoko hapo. Hospitali za maskini ni hospitali za *Panadol*, dawa ya maumivu tu, maana hawana dawa zingine. Wakienda katika hizi hospitali, iwapo wana kesi nyeti, ni lazima waletwe Nairobi. Hospitali ya Kitaifa ya Kenyatta ina madaktari 264. Wale ambao wanasimama pale *casualty* kwa matibabu ya dharura ni sita. Kwa mfano, Hospitali ya Coast General inapokea zaidi ya watu 50 kwa siku moja kutoka kaunti mbalimbali waliotumwa kwa sababu vifaa ama huduma inapatikana huko. Hospitali ya Kitaifa ya Kenyatta inapokea kati ya watu 200 na 300 kila siku kutoka sehemu mbalimbali sawia na ile ya Eldoret.

Mwaka wa 2015/2016, Serikali ya Kenya ilitumia Kshs.38bilioni kwa mashine za kisasa katika hospitali lakini kwa sasa hazifanyi kazi, kwa sababu hatuna madaktari wanaopata mafunzo ya kuzitumia. Mwaka uliopita 2015/2016, ilianguziwa katika vyombo vya habari ya kwamba mashine za kisasa za saratani na figo zimekuja. Watu walifurahi na wakasema kweli ugatuzi umezaa matunda. Ugatuzi wakuleta mashine bila daktari wa kujua kuzitumia nikutia gunia upepo kwa maana haina faida. Ninaposema kutia gunia upepo na maanisha ya kwamba unatia gunia upepo lakini linatoa. Kwa hivyo, haujazi. Inakuwa ni kazi ya bure. Je, kujenga hospitali moja ya rufaa katika kaunti moja itagharimu Serikali pesa ngapi? Itagharimu takriban Kshs3bilioni. Tukisema tuboreshe zile zilizopo ambazo nimezitaja kutoka Level 5 hadi Level 6, tunaweza tumia Kshs2bilioni. Sasa wacha nikupe mfano tufanye hesabu. Kujenga hospitali moja ni Kshs3bilioni. Kuboresha hospitali iliyoko ni takriban Ksh2bilioni. Idadi ya Wakenya wanaondoka nchini kuenda kutafuta matibabu nje hususan taifa la India, kila mwaka wanatumia Kshs10bilioni. Ni jambo linaweza kufanyika. Idadi ya watu wanaokufa inazidi kuongezeka. Mungu ametujalia tumeletwa katika Bunge hili kujadili na kutunga sheria, lakini hatutungi sheria ambazo zitatulinda pia sisi tukitoka, maana hakuna mtu atakayeishi hapa milele. Tukitoka hapa, vizazi vyetu hatujui kama vitakuwa vya ubunge, kula madawa ya kulevya ama kuiba. Watakuwa ni miongoni mwa wale ambao watapata matatizo ambayo sisi tunasuluhu sasa hivi. Nitakupa mifano nikianzia na mgomo uliofanyika miezi minane iliyopita, wakati madaktari waligoma. Nitakupa tu mifano na kaunti kadhaa kama Kaunti ya Kilifi.

Kaunti ya Kilifi ina madaktrari wa upasuaji wa *caesarean section* 18. Ina madaktari wa upasuaji 18 peke yake. Idadi ya vitanda ni 610. Wagonjwa wanaokwenda kutibiwa kila siku ni zaidi ya 10,852. Watu wanaokufa ni 1,410. Wanakufa kwa sababu ya magonjwa ya kiajabuajabu. Magonjwa yanayo tiba lakini tunayachukulia mzaha mzaha. Leo, Mombasa tunakufa kwa sababu ya Chikungunya; eti ukiumwa na mbu, wewe kwisha. Hatuna wataalamu wa kupambana na magonjwa. Maradhi ya ajabuajabu yanatokea na hatuwezi saidika. Asilimia kubwa ya Wakenya hata hawana ile Bima ya Afya ya Kitaifa. Hawawezi kujitetea na hawajui la kufanya.

Angalia Kaunti ya Mombasa. Idadi ya wanaokufa ni 1,272. Katika miaka ya 2014 na 2015, Kilifi ilifanyia upasuaji wagonjwa 2,668. Waliokufa ni 1,553. Haikubaliwi. Inasemekana kwamba kila nafsi itaonja mauti, lakini suala la kuonja mauti kwa sababu ya udhalimu na uzembe wetu sisi Wabunge halikubaliki. Sisi ni wasomi ambao tuko na *Bachelor's Degree* na *Master's Degree* lakini tumeamua kuweka makaratasi yetu kwenye mifuko na kushabikia ukiritimba. Hili leo nalipite ili tuweze kupata hospitali katika kila kaunti Kenya nzima.

Bado nitaendelea kulilia hili suala kwa sababu linahusu mwananchi wa kawaida. Nitazungumzia hospitali na vile vile madaktari wenyewe. Katika Kenya ya sasa, madaktari ambao tunawategemea wanalipwa mishahara ambayo haiingii akilini. Nitaanza na ile wanaita *entry level*, ambayo ni hatua ya kwanza ya daktari kuingia. Mshahara wao wa kwanza wakimaliza mafunzo ni Kshs44,000. Daktari aliyekaa katika taaluma hiyo kwa muda wa kati ya miaka 10 na 15 – daktari ambaye anakuangalia tu hivi na anajua dawa yako – analipwa Kshs114,000 katika Kenya ya sasa. Ndio unaona tumekuwa na uhaba wa madaktari. Wengi wao wanakimbia kwenda kufanya kazi nje. Wengi wanafungua hospitali zao za kibinafsi ambazo haziwezi kufikiwa. Daktari aliye na uzoefu wa zaidi ya miaka 15 analipwa takriban Ksh200,000. Watu wanaumia na wanakufa. Sisi tuna uwezo.

Mungu hatusamehi sisi Wabunge kwa sababu tukiwa wagonjwa tuna suluhu. Sisi tunaenda katika mahospitali ya kifahari. Tunapanda ndege na kuenda Ulaya kutafuta matibabu lakini Mungu anaturegesha katika majeneza na masunduku hadi nchini Kenya. Kisha tunaanza kupiga kelele na kusema kwamba ni vipi Mbunge fulani alipelekwa nje aende apate matibabu amerudi akiwa maiti? Ni aibu. Hatuwezi kutunga sheria za kuleta hospitali, usawa na haki? Leo sisi tunasikia uchungu mmoja wetu akituondokea kwa sababu tumejaribu kila tuwezacho. Tumetumia pesa, tumemwaza Nairobi Hospital, Aga Khan Hospital, tumempandisha ndege, ameenda Uingereza na Marekani lakini hivyo hivyo, amerudi akiwa maiti ndani ya sanduku. Yule mama anayeuzua mboga kule Kaloleni, Giriama; yule mama anayeuzua viazi kule Nyeri; yule mzee ambaye anakaa kule mashinani Turkana na Pokot; ni nani anayempeleka katika hizi hospitali? Ni nani anayemkatia nauli ya kupanda ndege na kuenda Ulaya? Hakuna? Atakayefanya hiyo kuhakikisha ya kwamba watu hawa hawatapata haya matatizo ni sisi Wabunge wote. Kwa kauli moja, tukubaliane ya kwamba hii ina umuhimu zaidi na ni ya Wakenya asilimia 80 ambao hawana huduma za afya.

Leo nchini Kenya, miaka 55 baada ya kupata Uhuru, mama anajifungua ndani ya nyumba. Jamani hatuoni haya? Jamani hatuogopi Mungu? Mama anakufa akijifungua mimba kwa sababu hawezi kufikia hospitali. Mfano ni katika Eneo Bunge la Nyali, ninakotoka. Linaonekana kama eneo Bunge tajiri kwa sababu ukisema unaenda Nyali watu wanajua ni Eneo Bunge tajiri. Lakini utashangaa nikikuambia kwamba Mungu anajalia akina mama wetu kupata mimba ndani ya Nyali lakini wanajifungua katika Eneo Bunge la Mvita. Hali hii haikubaliki.

(Laughter)

Jameni, hili si jambo la kuchekea wala kushabikia. Watu wanakufa. Leo maradhi madogo madogo yanatusumbua. Nimekupa mfano wakati nilipoanza mjadala wangu. Naona muda unanipa kisogo. Ningelipenda kusoma na kuelezea mengi zaidi lakini kwa hayo machache naomba ya kwamba haya yamewaingia Wabunge.

Naomba kuwasilisha Hoja hii na atakaye afiki, yani *Seconder*, ni Mheshimiwa Kanini Kega.

The Temporary Deputy Speaker (Hon. (Ms.) Mbalu): Nampa nafasi Mwafiki.

Hon. Kanini Kega: Asante Mheshimiwa Naibu Spika wa Muda.

Hon. Wakhungu: On a point of order, Hon. Temporary Deputy Speaker.

The Temporary Deputy Speaker (Hon. (Ms.) Mbalu): Mheshimiwa Chris Wamalwa, Hoja inaaafikiwa.

Hon. Wakhungu: Hoja haijwasilishwa kikamilifu katika ule mnyambuliko ambao Mheshimiwa amesema.

Unapokuwa na Hoja ni lazima useme “*I beg to move*” yani “nasongesha”.

(*Laughter*)

Lakini labda mwenzetu amesahau sheria na tamaduni za Bunge. Ukileta Hoja ni lazima “usongeshe”. Mwenzagu amesahau “kusongesha”. Lazima “asongeshe”.

The Temporary Deputy Speaker (Hon. (Ms.) Mbalu): Mheshimiwa Christopher, kama Spika, nimemsikiza vizuri Mtoa hoja. Alipokuwa akimaliza, alisema kuwa angeomba kuwasilisha Hoja hiyo. Hiyo inamaanisha “*I beg to move*”. Amesema anaomba kuwasilisha Hoja na akamwita atakayeafiki, yani *Seconder* ambaye ni Mheshimiwa Kanini Kega.

Hon. Kanini Kega: Asante sana, Mheshimiwa Naibu Spika wa Muda kwa kunipa nafasi hii ili niafiki Hoja hii ambayo imeletwa na rafiki yangu, Mheshimiwa wa Nyali, Mohamed Ali, ambaye tunamjua sana kwa jina “Jicho Pevu”. Tunafurahia kwa sababu Hoja ambayo amewasilisha hapa ni muhimu sana, na yale aliyoyaangazia ni mambo ambayo yanaathiri watu wetu kila uchao.

Lakini wakati Mhe. Ali jana alipokuwa anatoa Hoja hii, angetoa ilani kwa Wabunge kwamba leo tutakuwa tunaongea kwa Kiswahili ndiyo watu waweze kubeba kamusi. Nimeona sana wakati Mheshimiwa alikuwa anaendeleza Hoja hii, wengi walikuwa wameachwa vinywa wazi. Hawakuwa wanaelewa, hasa sisi ambao tumetoka bara. Lakini nitajaribu nione kama nitaweza kuiafiki Hoja hii kulingana na matarajio ya Mhe. Mohamed Ali.

Tutakumbuka kwamba wakati tulipoanzisha serikali za ugatuzi mwaka wa 2013, tuliona sana magavana wengi wa nchi hii wakikimbia kununua magari ya kusafirisha wagonjwa yanayojulikana kwa kimombo kama *ambulance*. Walikuwa wanazinunua ili wakipata wagonjwa katika sehemu zao, waweze kusafirishwa mpaka kwenye hospitali kuu hapa Nairobi na kule Eldoret.

Kuhusu uzima wa mwili, yani *health*, kwa maoni yangu, tulikosea kidogo wakati tulipoigatua sekta hiyo. Labda sekta hiyo ingeshikiliwa na Serikali ya kitaifa, haswa tukizingatia kwamba kila kuchao sisi, kama Wabunge, tunaitwa kushirika kwenye mikutano ya kuchangisha pesa. Hizo fedha tunachanga kila siku ni za kupeleka wagonjwa hospitali, ama ni za kugharamia kuzikwa kwa maiti? Vifo vingi vinavyotokea katika taifa hili husababishwa na magonjwa ambayo yanaweza kutibiwa ama kuhudumiwa kabla ya kusababisha vifo. Haya magojwa yatatibiwa namna gani ilihali hatuna hata zahanati? Yatatibiwaaje kama hatuna madaktari na waauguzi? Yatatibiwaaje kama madaktari tulionao nchini... Tuna madaktari ambao wanahitimu

kila mwaka kutoka vyuo vikuu. Lakini wakihitimu hawakai humu nchini. Wanahamia nchi za kigeni. Wanahamia nchi jirani na wengine nchi za Ulaya kwa sababu wanapata lishe bora huko.

Mhe. Naibu Spika wa Muda, naomba sisi kama Wabunge lazima tufanye kazi yetu sawasawa na tuhakikishe kwamba waliotuchagua, walituchagua tuwashughulikie kiafya, ajira na mengine. Mhe. Mohamed Ali alisema hospitali za rufaa ni muhimu sana. Tuko na mbili, moja hapa Nairobi na ingine kule Eldoret. Tukiangazia maeneo ya uwakilishi Bunge, hasa nikitoa eneo langu la Bunge kama mfano, hatuna hospitali ya kiwango cha 4, hata hospitali ya kiwango cha 5. Tuko na zahanati peke yake. Wagonjwa kutoka eneo langu la uwakilishi Bunge wanasafirishwa zaidi ya kilomita 200 ili wapate huduma za afya. Lazima tuimarisha zahanati tulizonazo kule mashinani ili zile za kiwango cha 4 ama kiwango cha 5 zihudumie wagonjwa ambao hawapati huduma kule mashinani.

Hili si jambo la mzaha. Ni jambo tunapasa kuangazia sisi sote pamoja na magavana. Naomba ya kwamba Hoja kama hii iwasilishwe katika gatuji zote za taifa hili. Ni jukumu la serikali yoyote kuhakikisha kwamba wananchi wake wote wako na afya njema. Uzima wa kimwili ni jukumu la ugatuji. Tukiwa na hospitali ya kiwango cha 6 katika kila gatuji... Hospitali ya Rufaa Kenya imekuwa na changamoto juzi. Wakati mwingine huwezi kulaumu madaktari kwa sababu kila siku wanafanya oparesheni nyingi kwa sababu wagojwa ni wengi na hatuna hospitali za kutosha. Tukiwa na hospitali za kiwango cha 6 kule Homa Bay, Nyeri ama Mombasa ama kwa gatuji zote 47 nchini, tutakuwa tumewashughulikia wananchi.

Sitaki kupitisha hapo. Kama Wabunge tuko na bahati maanake tuko na bima ya afya. Inatushughulikia kwa kutuwezesha kuenda kutibiwa kule ng'ambo. Lakini walalahoi wa kule mashinani wakigojeka ama wakipata magojwa ambayo hayawezi kutibiwa humu nchini, watafanya nini?

Naiafiki Hoja hii. Haitakuwa Hoja tu, tutahakikisha imetimizwa na Serikali ya Kitaifa na pia serikali gatuji.

Kwa hayo machache, naomba niketi. Asante sana.

The Temporary Deputy Speaker (Hon. (Ms.) Mbalu): Asante sana Mhe. Kwa kuafiki Hoja.

(Question proposed)

Waheshimiwa Wabunge, kabla hatujaendelea nimefurahishwa na Mhe. Wamalwa aliposema angependa Hoja isongeshwe, kumaanisha "*I beg to move.*" *That is literal translation.* Inafahamika kuwa "kuwasilisha Hoja."

Hon. Members, I would like to refer you to Standing Order No.77 which stipulates that:

"(1) All proceedings of the House shall be conducted in Kiswahili, English or in Kenyan Sign Language.

(2) A member who begins a speech in any of the languages provided for under paragraph (1) shall continue in the same language until the conclusion of the Member's speech."

Kwa hivyo, ukianza kutoa mchango wako kwa lugha ya Kiswahili, utamalizia na Kiswahili.

Nampa nafasi hii, Mhe. Christopher Wamalwa.

Mhe. Wakhungu: Asante sana, Naibu Spika wa Muda kwa kunipa nafasi ili nchangie Hoja hii. Kwanza ningependa kumshukuru Mhe. Mohamed Ali Mohamed kwa kuwasilisha Hoja hii.

Hii Hoja ni muhimu sana kwa sababu tuko na hospitali za rufaa mbili Kenya nzima. Tuko na Hospitali ya Rufaa ya Mafunzo ya Moi ambayo inasaidia watu wakutoka eneo la Magharibi na eneo la Nyanza. Vile vile, tuko na Hospitali ya Rufaa ya Kenyatta.

(Several Hon. Members walked into the Chamber)

The Temporary Deputy Speaker (Hon. (Ms.) Mbalu): Order. Kuna Waheshimiwa wamekosa nidhamu. Tafadhali tutii kanuni za Bunge.

Hon. Wakhungu: Vile vile, tuko na Hospitali ya Rufaa ya Kenyatta ambayo inajali masilahi ya wagonjwa kutoka eneo la Kati, Nairobi na eneo la Mashariki. Vile vile, hii Hoja ya kuwa na Hospitali ya Rufaa ya Kitaifa kule Mombasa itasaidia sana kwa sababu kuna wagonjwa wengi wanaotoka kaunti za Lamu, Mombasa, Kwale, Kilifi na Taita Taveta. Ukiangalia ajenda ya jubilee, utapata kwamba matibabu yamepewa kipaumbele. Isitoshe, kuhusu Malengo Endelevu ya Maendeleo, hasa lengo la tatu (SDG-3), mambo ya *universal healthcare* yamezingatiwa. Mwenzangu Mohamed Ali ameongea kiswahili mufti. Tulijaribu kumfuatilia ikawa vigumu lakini katika zile pilkapilka za kumuelewa tukagundua kwamba tunaendelea kujifunza kidogo kidogo.

(Laughter)

Wajua kwamba Kiswahili ni lugha ya taifa. Mimi naomba tutenge angalau siku moja ili Wabunge waongee Kiswahili. Hii ni kwa sababu wakati tunaongea Kiingereza hapa, yule nyanyangu aliye nyumbani haelewi tunachosema. Kulingana na Katiba mpya, mambo ya Bunge lazima yajadiliwe hadharani ili mwananchi wa kawaida afuatilie na apeane mawaidha yake.

Nikimalizia, yafaa tutenge pesa katika Bajeti kwa sababu mara kwa mara Hoja nzuri kama hii zinaletwa hapa, tunazipitisha lakini hakuna mtu wa kuzifuatilia ili zitekelezwe. Sisi tukiwa Wabunge hatuwezi kupitisha Hoja na hiyo Hoja isitiliwe maanani. Ndiposa nimeangalia humu ndani nikamwona mwenyekiti wa kamati ya utekelezaji. Katika Kiswahili ni “implements honi”

(Laughter)

Hii Hoja ikipita, yafaa aifuatilie ili tuwe na Hospitali ya Rufaa ya Kitaifa kule Mombasa. Wengine labda wanasema Mombasa si Kenya. Sisi tunajua Pwani ni Kenya. Ni vizuri hospitali iwe hapo karibu ili iwasaidie akina mama, watoto na wagonjwa kwa ujumla. Wakenya wanatumia pesa nyingi kuenda ng'ambo kutafuta matibabu. Wengine wanaenda kule India ilhali matibabu wanayotafuta huku yanapatikana hapa nyumbani. Ukienda kule Kenyatta, wagonjwa wamejaa sana. Tukitaka hospitali ya Kenyatta isiwe na wagonjwa wengi, lazima tuanzishe hospitali nyingine za rufaa. Kule Eldoret, kuna Hospitali ya Rufaa na Mafunzo. Tunataka hospitali ya rufaa kule Mombasa ijengwe ili wagonjwa wa saratani waende pale. Vile vile, upasuaji utafanywa pale.

(Hon. Mbadi withdrew from the Chamber)

Mhe. Mbadi amesema kulingana na kule anakotoka hawezi kuongea kiswahili maana ni kigumu sana.

(Laughter)

Amesema anataka anione nikijetetea kidogo kidogo. Nikiweza ataongea, na akiona kinanilemea basi ataondoka. Ninajua watu wangu wa Kiminini wanafurahi kwa sababu wanasikia na wanaelewa Kiswahili. Wale wako nyumbani vile vile wanafurahi wakisikia tunaongea kiswahili. Watu wengi nchini wanaelewa Kiswahili.

Tunaiomba ile Kamati yetu ya Bajeti kwamba ikileta Bajeti ya Ziada hapa, lazima tutenge pesa ili zitumike katika ujenzi wa hospitali ya rufaa. Hatutaki tupitishie Hoja hii na ikose kutekelezwa. Nilikuwa na mengi ya kusema lakini wacha nikomee hapo ili wengine vile vile waongee. Ninashukuru Mhe. Mohamed Ali kwa kuleta hii Hoja. Ninaunga mkono.

Ahsanteni sana.

The Temporary Deputy Speaker (Hon. (Ms.) Mbalu): Ningependa kumpa nafasi mwakilishi wa Eneo Bunge la Westlands, Mhe. Wetangula Wanyonyi.

Hon. Wetangula: Ahsante sana, Mhe. Naibu Spika wa Muda, kwa kunipa nafasi hii ili nami pia nichangie Hoja hii ya Mhe. Mohamed Ali ambaye kwa umaarufu anaitwa “Jicho Pevu.”

Hii ni Hoja ya maana sana. Katika nchi hii yetu, miaka 54 tangu tujinyakulie uhuru, suala la afya bado linatuchanganya. Tunatumia pesa nyingi sana kupeleka wagonjwa katika nchi za nje kutafuta matibabu. Hizi pesa zinaweza kutumika katika nchi hii kujenga hospitali ambazo zinaweza kuwa na vifaa maalum. Tuko na madaktari ambao wamehitimu katika nchi yetu wanaoweza kufanya kazi katika hizi hospitali. Ukienda Hospitali Kuu ya Kenyatta, utapata kwamba haina vifaa vya kisasa. Hii ni aibu kubwa. Madaktari wapo lakini wale wanafanya upasuaji wanafanya kazi katika mazingira duni kabisa. Lazima tuweke maanani mambo ya afya kwa sababu nchi ambayo haina afya haiwezi kuendelea. Nchi ambazo zimeendelea zimetilia mkazo sana mambo ya afya.

Kitu kingine ni kwamba matibabu katika nchi yetu ni ghali sana. Watu wanalipa pesa nyingi. Ndiyo maana unapata watu wanakufa kwa magonjwa ambayo yanaweza kutibiwa. Wagonjwa wengi hawawezi kufika hospitali ama wakifika hospitali huwa hakuna madawa. Lazima Serikali ikeze pesa katika mambo ya afya ili tulipe madakdari vizuri, tununue vifaa, tuweke madawa katika hospitali na tujenge hospitali za kisasa katika kila kaunti, vile Mhe. Mohamed amesema. Tuko na kaunti 47. Kaunti nyingi hazina hospitali za kiwango cha 4 yaani Level 4. Nyingi ni hospitali ndogo ambazo hazina vifaa vya kisasa.

Karibu miaka 20 iliyopita nilipopata ajali, nilipelekwa Brussels, Ubelgiji kwa matibabu. Nikienda huko, nilifikiria ninaenda kupata matibabu ambayo hayawezi kupatikana hapa Kenya. Nilipofika huko, niliona mambo ya kawaida ambayo yanafanywa hapa Kenya. Kwa sababu hatuna hospitali ya kiwango cha juu, singepata hayo matibabu huku kwetu. Mimi ninajua kuna wakenya wengi ambao wanapata ajali katika barabara zetu na hawawezi kufika hospitalini kwa sababu ni ghali na hakuna vifaa vya kusaidia wagonjwa ambao wamepata matatizo ya uti wa mgongo ama wale wa saratani. Ukienda hospitali za kibinafsi kama Aga Khan ama Nairobi utapata wako na vifaa vya kisasa ambavyo vinaweza kutibu aina yote ya magonjwa lakini ni wakenya wangapi wanaweza kufika katika hizo hospitali?

Kwa hivyo, hii Hoja itawezesha kujengwa hospitali ambazo zitafikiwa na wananchi wa kawaida. Vile vile, Serikali inatakikana iangalie gharama ya matibabu kwa sababu matibabu katika zile hospitali za umma inashinda watu. Watu wakienda huko, daktari anawaandikia dawa ama vifaa vya kununua ili warudi kutibiwa. Hiyo haiwezekani kwa sababu wananchi wengi wana

matatizo mengi. Kuna umaskini na tunatakikana tuangalie kwamba watu wanapata matibabu badala ya kuambiwa waende watafute matibabu pahali pengine.

Tukijadili hii Hoja, tunatakikana tuifanye sheria katika nchi yetu ili tuanze kufikiria ni namna ipi tutainua viwango vya mahospitali ili tuwe na hospitali ya Level 5 katika kila kaunti; iwe na vifaa vya kisasa, dawa na ile huduma ya madaktari kutumwa huko. Kila wakati tuna migomo ya madaktari. Madaktari wa Hospitali ya Kenyatta wamefanya upasuaji hivi juzi na kutibu mtoto ambaye mkono wake ulikuwa umekatika lakini hakuna mtu anawatambua. Wakifanya kosa kidogo, utaona kila mtu anawaelekezea kidole cha lawama. Madaktari wanang'ang'ana kufanya kazi katika mazingira duni. Lazima tuangalie ni vipi tutafanya bidii tuweke kiwango cha hospitali zetu kiwe katika hali nzuri.

Nashukuru sana Muwasilishi wa Hoja hii, Mhe. Mohamed. Naomba Wabunge wenzetu wachangie na kuunga mkono. Mhe. Naibu Spika wa Muda, naomba kusema asante kwa Hoja hii na kunipa nafasi kuchangia; asanteni sana.

The Temporary Deputy Speaker (Hon. (Ms.) Mbalu): Asante Mheshimiwa wa Westlands. Waheshimiwa, ningependa kuchukua nafasi hii kuwakaribisha wanafunzi kutoka shule ya Kamuwongo Day Secondary School walio katika Public Gallery. Iko katika Mwingi North Constituency, Kyuso Ward, Kitui County. Wako na Mheshimiwa wao, nimeona yuko ndani ya Bunge; Mhe. Paul Nzengu. Karibuni.

(Applause)

Ningependa kutoa nafasi kwa Mheshimiwa wa Kaunti ya Narok, Mhe. Tuya Soipan.

Hon. (Ms.) Tuya: Asante sana Mhe. Naibu Spika wa Muda kwa kunipa fursa hii kuchangia Hoja hii nzuri sana.

Ningependa kuanza kwa kumpongeza Mtoahoja, Mhe. Mohamed Ali Mohamed. Nilipokuwa nikimsikiza akiwasilisha Hoja hii, niliona kwamba alipoingia kwenye siasa, lile jicho lake pevu bado liko pale pale. Nasema hivi kwa sababu amewasilisha Hoja ambayo ameifanyia utafiti wa kutosha na kutupa njia muafaka ambayo kila mmoja ambaye anajali afya ya waliotuchagua kuwa Wabunge wa Bunge la Kitaifa, bila shaka sote tutaunga mkono Hoja hii.

Nilipokuwa namsikiza Mhe. Ali na ukiangalia Hoja yake, haiangazii tu hali ya Kaunti ya Mombasa. Mtoahoja ametuelekeza kwa Kifungu cha 25 ambacho kinatukumbusha ya kwamba kuna lile azimio ambalo tumetoa tukiwa watungasheria au wanasheria la kuwa na maono ya kuhakikisha katika kila gatuji la nchi hii kuna ile Hospitali ya Kitaifa ya Kiwango cha 6.

Nikiunga mkono Hoja hii, nimekuwa mmoja wa wale wa Bunge la 11 ambao walihuzunishwa na kule kuweka maslahi ya afya yawe kwenye serikali za kigatuji na kuyaondoa kwa Serikali kuu. Sababu yangu ya kuona hapo hatukufanya vyema ni ukijaribu kuangalia mpangilio wa kazi wa kaunti zetu jambo la afya liko chini kabisa kwa orodha ya umuhimu katika kaunti zetu. Nilisikia mmoja wa Wabunge ambao waliongea mbele yangu akisema kwamba mipangilio ya magavana wengi wamekimbilia kununua yale magari ya dharura ama *ambulances*. Tayari hiyo inaonyesha yale mawazo yaliyo kwa magavana wetu. Wazo lao ni kwamba kile wanakipa kipaumbele ni njia ya kuwaondoa sehemu gatuji zao na kuwapeleka nje ya zile kaunti ili kupata matibabu. Hiyo inatuonyesha kwamba yale mamilioni ya pesa wameweka kwa kununua yale magari yangewekwa katika kuweka msingi ama kuweka hospitali zinazopatikana katika kaunti ziinuke kuingia kwa hali nyingine.

Katika Kaunti yangu ya Narok ambapo mimi ndiye mwakilishi wake, ukienda kwa ile hospitali kuu ambayo tuko nayo katika Kaunti ya Narok, hali yake ni ya kutatanisha zaidi.

Utakuta kuna daktari lakini mgonjwa akitaka kufanyiwa utafiti zaidi analazimika kutoka pale kwa hospitali kupelekwa na jamaa yake kutafuta pahali pa kutoa damu ili ipimwe kwingineko. Kununua dawa, inalazimika atoke kwa hospitali akatafute dawa kwingine. Nafikiri hiyo ni kuonyesha kwamba mipango yetu ama kwa lugha ya Kimombo *priority* zetu hatuzajiweka vizuri kama nchi.

Kifungu cha 43 cha Katiba yetu kinaruhusu ama kuweka wazi ya kwamba kila Mkenya anastahili kuwa na kiwango cha juu zaidi cha afya bora. Ni haki, si ndoto au kitu tunatarajia kupata. Kwa sasa, iko katika ile sehemu tunaita *Bill of Rights* ambayo kila Mkenya anahitajika kuwa nayo. Ukiangalia ule utafiti ambao Mhe. Mohamed ameufanya na kutuonyesha vifo ambavyo vinafanyika katika hospitali zetu za kaunti unaonyesha kwamba hali yetu ya afya inazidi kuzorota siku baada ya nyingine. Hata kama tungekuwa tunataka kufanya mabadiliko ya kidharura, bado nafikiria twahitaji kulifikiria jambo la afya; tuone kama tunaweza kulirudisha kwa Serikali ya juu ili liangaziwe na kupewa uzito unaostahili. Tukiendelea hivi, Wakenya watazidi kufa kiholela na kwa magonjwa madogo madogo ambayo yanaweza kutibiwa. Tutazidi kuona kwamba afya itakuwa inapatikana na wale ambao wanajiweza kiuchumi tu.

Hiyo si halali, ni kinyume na Katiba yetu. Hivi juzi, shida ilitokea katika hospitali kuu ya Kenyatta. Watu wakapata shida kule Garissa, Wajir na sehemu nyingi nchini, tumekuwa na shida nyingi za kiafya kama vile shida za akina mama kudhulumwa kwa njia mbalimbali. Tumaini waliyo nayo ni kutolewa kule waliko wapelekwe katika hospitali kuu ya Kenyatta. Wakati hospitali hiyo inapopata shida, kama kupata “homa” au “kupiga chafya”, Wakenya wote hupata “homa” na kila mmoja anaitegemea hospitali hiyo; pamoja na Hospitali ya Rufaa na Mafunzo ya Eldoret.

Hatuwezi kuendelea hivi. Umefika wakati ambapo tunafaa kujadiliana na kuliangazia suala la afya kwa lengo la kubadili mipangilio yetu katika sekta hii. Kwa hivyo, nampongeza Mhe. Mohamed, ambaye ndiye mwasilishi wa Hoja hili. Naunga mkono kubuniwa kwa hospitali ya kiwango cha sita kule Mombasa. Ninaomba juhudi hizo pia zifuatilishwe katika kila sehemu gatuzi humu nchini kwa sababu hiyo ndio sheria tunayotunga. Hivi sasa, sioni kama mtu yeyote anayefikiria vizuri anaweza kuipinga Hoja hii. Sisi sote tunaunga mkono. Hoja hii itashughulikiwa na Kamati ya Utekelezaji, si Kamati ya *Implementation* kama alivyosema, Mhe. Spika. Hii itahakikisha kuwa Hoja hii imeenda katika kiwango kingine ili kuhakikisha Hoja hii...

The Temporary Deputy Speaker (Hon. (Ms.) Mbalu): Asante sana Mhe. Soipan kwa kuchangia Hoja hii iliyowakilishwa Bungeni na Mbunge wa Nyali, Mhe. Mohamed Ali. Ningependa kumpa fursa hii Kiongozi wa Walio Wachache Bungeni.

Hon. Ng'ongo: Asante sana, Mhe. Naibu Spika wa Muda. Ningependa kuchangia Hoja hii.

Kwanza kabisa, ningependa kumkosoa mwenzangu, Mhe. Wamalwa, ambaye amesema sina uwezo wa kuzungumza Lugha ya Kiswahili. Pengine sina uwezo wa kuzungumza Lugha ya Kiswahili sanifu lakini nina uwezo kama Mkenya mwingine yeyote kuzungumza Lugha ya Kiswahili, kwa sababu hii ni lugha ya taifa. Pia ningependa kuwajuliza kwamba mimi nilisomea Lugha ya Kiswahili hadi kidato cha nne. Nilipitia katika somo la Kiswahili. Nilipokuwa nikiwania kiti cha Bunge, wawaniaji wenzangu walifanyishwa mtihani wa Lugha ya Kiswahili; lakini mimi nilipewa ruhusa kwa sababu nilifanya mtihani wa Lugha ya Kiswahili katika kidato cha nne. Kwa hivyo, si kweli kwamba Mhe. Mbadi hawezi kuzungumza Lugha ya Kiswahili.

Sasa ningependa kuchangia Hoja iliyoko mbele yetu. Kwanza, ningependa kushukuru mwenzangu, Mbunge wa Nyali kwa kuileta Hoja hii Bungeni. Katika Kifungu cha 43 cha Katiba yetu, afya imepewa uzito zaidi. Kifungu hiki kinasema kwamba kila Mkenya ni lazima apate

matibabu ya kiwango cha juu zaidi ambayo yanaweza kupatikana humu nchini. Kwa sababu hiyo, inatajikana tuangalie sana sekta hii, kama nchi.

Nimesikia wenzangu wakisema kwamba pengine sisi kama Wakenya tulifanya makosa kupeleka sekta ya Afya kwa serikali za ugatuzi. Natofautiana nao kwa sababu ugatuzi ulikuja hivi juzi tu; mwaka wa 2013. Kabla ya ugatuzi, huduma za afya zilikuwa chini ya Serikali ya kitaifa kwa zaidi ya miaka 50, na kupata huduma za matibabu ilikua shida sana. Hii ndiyo sababu sisi Wakenya tuliama huduma hii ni lazima iwekwe kwenye serikali za ugatuzi ili sisi wenyenye kule mashinani tuone jinsi tutakavyoshughulikiwa. Haistahili tuwe na hospitali ya kiwango cha sita Mombasa pekee. Kama Wakenya, inatajikana tuliangazie suala hili kwa nia nzuri na tutafute fedha ili tujenge hospitali za kiwango hicho katika maeneo yote humu nchini; yakiwemo Kisumu, Kakamega na hata Garissa, ili watu wetu wakipata magonjwa yasiyoweza kutibiwa katika hospitali za kawaida, waweze kutibiwa haraka na karibu.

Ningependa kuwahimiza Waheshimiwa wenzangu kuunga mkono Hoja hii, na pia tuifuatilie. Tusiipitishie tu halafu ikuwame hapo tu. Kamati ya Bunge husika iko na jina gumu sana. Nilimsikia mwenzangu akijaribu kuibatiza kamati hiyo jina la “implementsioni”. Ni Kamati ya Utekelezaji. Tunamuomba mwenyekiti wa kamati hiyo, tutakapoipitisha Hoja hii leo ama baadaye, wahakikishe kwamba maombi ya mwenzangu yametekelezwa.

Mhe. Naibu Spika wa Muda, ninaunga mkono.

The Temporary Deputy Speaker (Hon. (Ms.) Mbalu): Asante sana, Kiongozi wa walio Wachache Bungeni, Mhe. Mbadi. Nina maombi 37.

Allow me to speak in English so that we can all communicate. That way, those who are still learning Kiswahili can understand. Standing Order No. 77 is clear on the proceedings of the House. All Members are equal in this Parliament. Let us allow the Speaker to execute her duties. Tutafikiwa sote.

Ningependa kumpatia Mhe. Opiyo, Mwenyekiti wa Kamati ya Uchunguzi wa Hesabu za Serikali, fursa hii.

Hon. Wandayi: Hon. Temporary Deputy Speaker, I do not want to pretend that I can speak good Kiswahili. Therefore, I will proceed in English, if you allow me. Of course, I know I am in order to speak in English on this Motion.

At the outset, I wish to support this Motion. I support it largely in principle. I will explain why. It is clear that health is a very critical issue to all citizens, particularly to those citizens who are not well endowed to afford the high cost of healthcare we have come to associate our country with. It is a good intention to have Level 6 hospitals – what we are calling national referral hospitals – established in each of the 47 counties. It is a good intention and dream.

Hon. Temporary Deputy Speaker, even before we get there, this Motion is about creating a referral hospital in Mombasa County. I know all the other counties apart from Nairobi and Uasin Gishu which have referral hospitals currently, equally deserve to have this kind of hospital.

It is true and we are aware that it will take some time before each of these counties gets to that stage. That is when you want to face reality because of the obvious constraints. But even as we aspire and walk towards that level, as a country, we should have put more emphasis in ensuring that the existing health facilities at the grassroots – one can call them sub-county hospitals or dispensaries - those facilities that currently exist, are properly and adequately equipped with facilities. They should have equipment and the right personnel to offer primary

healthcare. These are the vary services the Kenyan people are yearning for. We face the problem of unaffordable or inadequate primary healthcare services.

Hon. Temporary Deputy Speaker, we are aware that the function of health is largely devolved. I support what my chairman has said. I do not think that we should try and take back the function of health from the counties to the national level as a way of addressing the problem we are facing in that sector. That will be skirting around the problem. We should be asking ourselves what it is that has made it impossible or difficult for the county governments to perform this very critical function of health. For you to prescribe solutions to a problem, you must, first of all, carry out a proper diagnosis. Why is it that for more than six years upon the advent of devolution our county governments are unable to perform the health function in the manner Kenyans expect them to? Is it that this function was taken to them prematurely or it is because of inadequate resources to support it? What is it? That is the question we have to answer even as we strive to establish level 6 hospitals in our counties. Again, a level 6 hospital, as the name suggests, is a referral hospital. It is only for referral cases yet the majority cases that we have to deal with are primary healthcare cases that need not have to go to those referral hospitals in the first place.

Until recently, the Kenyatta National Hospital was actually changed from being a referral hospital to a primary healthcare institution which was not the original intention. It happened because those health facilities that needed to provide primary healthcare services were unable to do so. We can create another hospital in Mombasa, Bungoma or God willing in Siaya County where I come from and transform them into basically primary healthcare facilities on account of the fact that those facilities which need to provide these primary healthcare facilities are not able to do so. So, this House has a challenge to rise to the occasion and confront this problem holistically. Otherwise, the approach we are taking is not going to help provide a long term solution.

I want to fully support my friend, Hon. Mohamed Ali for bringing up this Motion, if only to jolt and awaken us that there is something that needs to be done, if we are to save the country from a catastrophe.

Hon. Temporary Deputy Speaker, it is known that Kenya has no shortage of properly trained health personnel. Kenya actually trains many health professionals and experts in nearly all areas of health or medicine yet we are unable to absorb all these personnel because we cannot afford to pay them adequately. That is why you find many highly trained doctors are leaving the country to go and offer their services elsewhere; services which we barely need as a country. Secondly, even for those who choose to stay around and support or serve Kenyans find it difficult to operate because of the poor working environment. From a policy point of view, this is an issue that requires relooking into holistically as I said earlier on. This House has a standing Departmental Committee on Health with has very competent Members and a Chairperson. So, they have a challenge to make a difference in this 12th Parliament. The country will be looking upon that Committee to provide a roadmap towards addressing this problem that we seem to be skirting around, first as a House, and second as a country.

Hon. Temporary Deputy Speaker, without belaboring the point, I wish to support. Thank you.

The Temporary Deputy Speaker (Hon. (Ms.) Mbalu): Thank you, Hon. Wandayi. Hon. Korere, the Floor is yours. Please use the other microphone or the Dispatch Box.

Hon. (Ms.) Korere: Shukrani, Naibu Spika wa Muda. Ningependa pia kumpongeza Mhe. aliyewasilisha Hoja hii, Mhe. “Jicho Pevu”. Kwa kweli, yeye ni jicho pevu mkakamavu.

Mhe. Naibu Spika wa Muda, ni wazi kwamba jinsi mienendo na mitindo ya kimaisha inavyobadilika, kumekuwa na changamoto nyingi sana hasa za kiafya. Kwangu binafsi, tungekuwa na uwezo wa kurudisha masaa nyuma tungelipitisha Hoja hii juzi. Waswahili husema kuwa “Hayawi hayawi huwa.” Kwa hivyo, ninaonelea kuwa ni Hoja ambayo wakati wake ni huu.

Mambo kuhusu afya katika nchi yetu ya Kenya yanatatanisha sana. Kama vile walionena mbele yangu walivyonena: Walalahoi, afya yao imeachwa mikononi ya Maulana. Pia, Mwenyezi Mungu aliweka tofauti kati ya binadamu na ng’ombe kwa kutupa akili kama ya kutibu ili tuitumie kisawasawa. Ni jambo la aibu kwamba Wakenya wengi wanakatika maisha mapema. Maisha ya wale ambao wanalinda familia zao yamekatika kwa ghafla. Wale wanaowategemea huachwa wasiwe na mbele wala nyuma. Hii ni kwa sababu gharama ya matibabu iko juu sana. Watu wanalazimika kuuza mifugo wao na hata mashamba ili kugharamia matibabu. Isitoshe, wagonjwa wanapoaga dunia, wanaobaki huwa hawana mbele wala nyuma.

Wabunge katika Bunge hili watakubaliana nami kuwa kila Ijumaa tunaitwa katika michango hapa na pale kwa ajili ya kuchangia wagonjwa. Kwa hivyo, Hoja hii aliyowasilisha Mheshimiwa “Jicho Pevu” ni Hoja ambayo imewasilishwa wakati bora na itatulazimu tuache shughuli nyingine zote ili tuipitishwe; kisha tuhakikishe imetekelezwa.

Mheshimiwa Naibu Spika wa Muda, jimbo la Mombasa anakotoka mwanzilishi wa Hoja hii, ni jimbo ambalo linasifika kwa utalii. Watu wengi ambao wanastaafu haswa wale ambao wanastaafu katika nchi nyingine na wanaathiriwa na baridi ya nchi zao, huja kupumzika kule Mombasa. Hawa ni watu ambao wako na taaluma tofauti tofauti wakiwemo madaktari. Tutakapokuwa na hospitali ya rufaa kule Mombasa, itasaidia pia watalii wagonjwa. Leo hii mtu akitoka Laikipia akitaka kutibiwa anaingia gari la moshi la *Standard Gauge Railway (SGR)* ambayo ililetwa na Serikali ya Jubilee, moja kwa moja mpaka Mombasa kutibiwa. Kwenda Mombasa si kama kwenda India kutafuta matibabu.

Cha kutia aibu sana ni kwamba katika Karne ya 21, akina mama wanakufa kwa ajili ya kujifungua. Katika hospitali zetu za majimbo bado hatujajimudu kuhakikisha kwamba akina mama wanapoleta maisha duniani humu, hawapotezi maisha yao. Kwa hivyo, tunapozungumzia mambo ya afya, ni sharti pia tuelewa kwamba taifa lenye afya ni taifa tajiri. Iwapo wale watu ambao sisi tunaongoza watakuwa wana afya njema, basi tutaweza kuwaambia vijana wetu wajitafutie riziki. Wataweza kufanya hivyo bila kuhangaishwa na maradhi.

Ni jambo la kutia hofu sana kwamba kila mara tunalia nchi haina fedha ilhali fedha nyingi zinapotelea katika miradi isiyofaa na yenye kufaidi watu binafsi. Hiyo ni miradi ya kuendeleza ufisadi. Ninazungumza bila kusita kwa sababu najua tulitenga fedha katika Bunge hili ili zitumike katika ugatuzi kwa kununua vifaa vya hali ya juu vya hospitali. Vifaa hivyo vilinuiwa kusaidia wagonjwa ambao wanalazimika kusafiri hadi Nairobi kupata matibabu. Kwa mfano, kusafishwa damu. Magonjwa kama vile kisukari, mpigo wa damu na saratani yamekithiri. Kwa hivyo, tuansema hivi: Iwapo kuna fedha zitatengewa masuala ya matibabu, basi fedha hizo zitumike vilivyo na kikamilifu kama alivyosema mwenye Hoja. Aliongeza kusema kwamba tumekuwa tukitia gunia pumzi. Baadhi ya majimbo, tunapozungumza sasa hivi, yamehifadhi mashine zilizogharimu mabilioni ya pesa katika mahospitali. Pesa zilizotumika si kwamba zimetoka kwenye mfuko wa mtu binafsi, bali ni kodi ambayo wamelipa Wakenya.

Kwa hivyo, itakuwa ni aibu kubwa sana kama kuna mashine ya kutibu wagonjwa na ambayo imehifadhiwa katika chumba mahali, pasipo kutumika... Kwa hivyo, ninapotia tamati ninaunga mkono Hoja hii. Shukrani na pongezi tena kwa aliyewasilisha Hoja hii ambayo tungepitisha jana na wala sio leo.

Ninapoenda kukaa, ningependa ieleweke kwamba mimi sitoki Pwani; ninatoka bara haswa eneo la Laikipia, - Mimi ndiye Mdorobo pekee katika Bunge hili. Mwalimu aliyenifunza Kiswahili katika shule ya upili ya Doldol, Bwana Mwangi Motisha, sasa ni mwalimu mkuu wa shule ya upili ya Miamoja; abarikiwe sana.

Shukrani.

The Temporary Deputy Speaker (Hon. (Ms.) Mbalu): Asante sana. Acha tumpatie Mheshimiwa Maanzo kutoka Eneo Bunge la Makueni.

Hon. Maanzo: Asante, Mheshimiwa Naibu Spika wa Muda, kwa kunipa muda wa kuchangia Hoja hii muhimu sana inayohusu mambo ya afya. Mheshimiwa Mohammed Ali Mohammed amafanya jambo la busara sana kuangazia mambo ambayo yanawahusu Wakenya wengi.

Kulingana na Katiba yetu katika Kifungu cha 43 na mpangilio wa kwanza wa sheria ya afya ya mwaka wa 2017, inaashiriwa kuwa kutakuwa na hospitali za kitaifa za rufaa za kiwango cha sita katika kila ugatuzi. Ni muhimu tulijadili suala hili na tuhakikishe limetekelezwa, kwa sababu kila sehemu ya ugatuzi nchini inafaa kuwa na hospitali kama ile ya kitaifa ya Kenyatta, ambayo sasa hivi inawashughulikia wagonjwa kutoka pande zote za nchi. Kuna hospitali nyingine kama hiyo kule Eldoret. Ni hizo mbili tu tunazo katika nchi yetu. Zitahitajika zingine 45 kote nchini.

Ningependa kuwapongeza magavana ambao wameshughulikia mambo ya afya na wamejaribu sana kutengeneza hospitali ambazo wako nazo. Mfano ni sehemu ya ugatuzi ya Makueni. Tumeshikana na Gavana wetu, Kivutha Kibwana ili kushughulikia mambo ya afya. Nimeona vile vile kuna magavana wengine ambao wanajaribu sana kuhakikisha kuwa afya imeendelezwa katika sehemu zao za ugatuzi. Hata hivyo, ni lazima Serikali kuu ihakikishe kwamba hospitali nyingine kama Kenyatta zimebuniwa na zimetengenezwa katika gatuzi tofauti tofauti. Sasa hivi hospitali ya Kenyatta inapokea watu kutoka kila mahali nchini. Imekuwa vigumu kuwasaidia wagonjwa wote katika hospitali hiyo. Hata ulinzi unakuwa ni shida kupeanwa.

Kuna mgonjwa mmoja kutoka Eneo Bunge langu la Makueni ambaye aliibiwa pale hospitalini katika sehemu ya kupokea huduma za dharura. Hii inamanisha kwamba hata ulinzi umekuwa changamoto.

Kwa hivyo, ni vyema Hoja kama hi iangaziwe. Aidha ni muhimu pesa itengwe kwa ajili ya masuala ya afya. Ikibidi, tutafute fedha kutoka kwa wafadhili ambao wanaweza kutusaidia. Hivyo, tutaweza kujenga hospitali katika magatuzi yetu likiwemo gatuzi la Mombasa. Kuna maeneo ya ugatuzi tofauti huko Pwani. Kuna Taita Taveta Kaunti na gavana wa huko anafanya juhudi kubwa ndiyo hata huko kuwe na hospitali kubwa, lakini fedha za kutosha hazijapatikana. Pia, kuna Kwale Kaunti na Mombasa Kaunti kwa Gavana Hassan Joho ambaye pia anaweka bidii lakini bado fedha hazitoshi. Vile vile, kuna Kilifi Kaunti na eneo hilo lote linatajikana liwe na hospitali moja kubwa haraka iwezekanavyo.

Lazima Serikali Kuu ifanye kazi na Mombasa Kaunti kuhakikisha kwamba hospitali hii inaanzishwa mara moja. Wafadhili wote na nchi zingine zote ambazo tunasaidiana nazo kuhusu afya na hata Shirika la Afya duniani, watusaidie ili mradi huu wa hii hospitali uanzishwe. Cha muhimu pia nikuangazia mambo ya maji safi. Maanake, tukiwa na maji ya kutosha magonjwa hupunguka kwa nusu. Dr. Sankok ako hapa na ni Mbunge ambaye anaelewa mambo ya afya. Ninatumaini kwamba hivi karibuni atachangia mambo haya kama mtaalamu anaelewa mambo ya afya zaidi kuliko mimi kama wakili. Lakini, bado naangazia haya mambo ijapokuwa siyafahamu sana kama Mhe. Sankok.

Ni lazima, tihakikishe kwamba wajuzi wa afya wanasaidia ili hospitali hiyo ya Mombasa iwe ya kwanza na zingine zifuata. Pia zile hospitali tuko nazo huko Embu na Nyeri zipandishwe na kufika kiwango cha Level 6, ndiyo watu wengi hapa Kenya wapate afya bora. Ni kweli, tunatumia fedha nyingi kwenda nchi za ng'ambo tukifuata matibabu. Tunawapelekea pesa zetu wataalamu wengine, ilhali, hapa Kenya tuna madaktari hodari sana ambao wameenda shule na kusomea mambo ya afya. Lakini, mpangilio wa kuwa na afya bora ndio umekuwa shida.

Pia, tuna madaktari hapa Bungeni lakini kiongozi wa Kamati ya Afya si daktari na Katibu wa Wizara ya Afya pia si daktari. Vile vile, hata Waziri wa Afya si daktari. Ingefaa, tuwe na madaktari katika huo mpangilio na kama ingewezekana Waziri wa Afya awe daktari ambaye anaelewa mambo ya matibabu. Lakini, kama ni mtaalamu mwingine ambaye haelewi ni nini huendelea katika hospitali, itamchukuwa muda na atachelewa kuelewa na wagonjwa wengi watapoteza maisha yao. Ni lazima, tihakikishe kwamba Wakenya wanatunzwa na tuna mpangilio mwema wa afya.

Tunaona Upinzani umesema kwamba tuwe na umoja na tusaaidiane ili Wakenya wote wapate Huduma zinazofaa. Kwa hivyo, nauunga Hoja hii mkono. Gavana wa Kakamega anajenga hospitali kubwa sana akitumia pesa za ugatuzi pamoja na zile za wafadhili. Ameonyesha bidii na magavana wengine wanafaa kumuiga. Vile vile, Gavana wangu Kivutha Kibwana anasonga mbele. Tunaona magavana wanafanya bidii na waungwe mikono ndiyo hospitali 47 ziweze kujengwa haraka iwezekanavyo.

Nashuruku na naomba kuunga mkono. Asante.

The Temporary Deputy Speaker (Hon. (Ms.) Mbalu): Asante, sana Mhe. Maanzo. Lugha yako ya mama yakaribia ile ya Mombasa, kwa sababu, eneo lako la Bunge la Kibwezi Mashariki liko karibu na barabara ya Mombasa. Mhe. Twalib wa Eneo Bunge la Jomvu.

Hon. Bady: Asante sana, Mhe. Naibu Spika wa Muda, kwa kunipatia fursa hii ili nami nichangie. Kwanza, naunga mkono Hoja hii kwa shauri ni muhimu sana. Vile vile, nataka kumpongeza jirani na ndugu yangu Mohamed Ali ambaye in Mbunge wa Nyali kule Mombasa. Tumetoka kaunti moja na amelea Hoja hii ambayo inapendekeza kuwa na hospitali ya rufaa katika mji wa Mombasa. Vile vile, sisi kama wanasheria katika kifungu cha 25 cha Sheria ya Afya, tumepewa nguvu ya kupendekeza kwamba katika kila gatuzi tuwe na hospitali ya rufaa ya kiwango cha sita.

Leo hii, mapendekezo hayo yatatusaidia. Kwa mfano, kule kwangu Jomvu kulitokea matatizo makubwa sana katika sehemu ya Owino Uhuru ambako kulikuwa na athari ya sumu. Tuliona huko Mombasa Kaunti kupitia Gavana Ali Hassan Joho walijaribu kuwatibu wananchi ambao waliathirika na hiyo sumu. Mpaka sasa, kwa shauri hakujakuwa na hospitali kubwa ya kuweza kuwatibu hao watu, bado athari hizo zimeongezeka. Leo hii, ukiangalia watoto ambao wanazaliwa, wengine wamedua. Pia wazee wanatamani kupata watoto wengine lakini mayai yao hayafanyi kazi vizuri. Kwa hivyo, watoto hawawezi kupatikana.

Kwa hivyo, Hoja hii ni nzuri sana. Tukiwa na hospitali ya rufaa tutaweza kutekeleza mambo mema kama yale ya ndugu yangu Mhe. Wamalwa ya utekelezaji. Utakuwa ni utekelezaji wa ukweli kupitia kwa kamati. Katiba yetu katika Kifungu cha 43 kinasema kwamba kila Mkenya ana haki ya kupata matibabu. Kwa hivyo, tukiwa na hospitali ya rufaa huko Mombasa haitatosha. Ni muhimu, hospitali hizi ziwe Kenya nzima ili tuone Wakenya wakiishi katika hali nzuri ya kuweza kupata matibabu kama haki yao ya kisheria.

Tumeona ndugu yangu Mohamed Ali amechanganua vizuri kabisa na kusema madaktari Kenya nzima ambao wamesajiriwa ni 11,000. Lakini, wale wanaofanya kazi ni karibu 6,000 pekee. Kwa hivyo, tukiangalia hali hii haiwezi kutupeleka mbele. Madaktari wako lakini

hawawezi kukimu yale mahitaji ya mamilioni ya watu ambao wako Kenya. Kwa hivyo, tukiangalia hali hii ya kuwa na madaktari wachache humu nchini, tunaona tunawapeleka wagonjwa hospitalini na baada ya siku chache tunawaona hao wagonjwa wakirudi katika hali ambayo si sawasawa.

Ndugu Mohamed Ali amesema kwamba, ni kweli Wabunge matumbo yakiwatokota kama vile mtambo wa kusaga unga, wanapata njia ya kuweza kukimbia ulaya na sehemu nyingine kwa sababu wana huduma za bima na mambo mengine. Vile vile, hata tumbo la Spika nalo likitokota kama vile mashine ya tuk tuk, vile vile anaweza kwenda ulaya kupata matibabu. Lakini mwananchi wa kawaida hawawezi kukimu matibabu hapa nchini. Kwa hivyo, pendekezo langu ni kwamba pesa ziende mpaka huko mashinani. Wale wote ambao hawawezi kulipia huduma ya kitaifa ya bima tuone kuwa watu hawa katika nyanjani wanaweza kulipiwa ili watu wote katika Kenya nzima wawe na bima. Tukiangalia katika ajenda kubwa nne za Serikali ya Jubilee ya Raisi Uhuru Kenyatta, hilo ni jambo moja ambalo wamelitia maanani sana.

Kwa hivyo, pendekezo langu ni kwamba, kwa sababu madaktari wetu ni wachache, wale wanaofanya katika mikataba waweze kuajiriwa kazi.

*[The Temporary Deputy Speaker
(Hon. (Ms.) Mbalu) left the Chair]*

*[The Temporary Deputy Speaker
(Hon. (Ms.) Tuya took the Chair)]*

Bi. Naibu Spika wa Muda, kwa vile madaktari wetu ni wachache, ninapendekeza wale ambao wanafanya kazi kwa kandarasi waajiriwe. Pia, ninapendekeza wahudumu wa kijamii katika sekta ya afya, yani *community health workers*, ambao wanafanya kazi katika hospitali zetu lakini hawajaajiriwa rasmi, waajiriwe ili waweze kuendelea kuwapa wananchi huduma.

Wiki mbili zilizopita, nilizungumzia kuhusu shida ya maji na leo naungana na ndugu yangu Mhe. Maanzo, kusema kwamba magonjwa mengi sana yanaletwa na shida ya ukosefu wa maji. Kama vile ilivyo katika Kipengele cha 43 cha Katiba yetu, kila mmoja ana haki ya kupata huduma ya afya. Vile vile, kila mmoja ana haki ya kupata maji safi katika nchi yetu ya Kenya. Jomvu kwangu watu wanaumia kwa sababu ya ukosefu wa maji safi. Ni muhimu sana tushikane na washikadau wote katika nchi hii kuona kuwa tumewapatia maji safi wananchi wetu ili hali yao ya afya iwe nzuri. Tusipofanya hivyo, katika kuwaelimisha watu wetu kuwa katika hali nzuri, kila watakapokuwa wagonjwa tukiwapeleka hospitali itakuwa ni kama vile ule msemo wa Kiswahili unaosema kuwa itakuwa “kirba goji, goji kirba;” yaani, twaenda humo humo na twajirudisha humo humo. Kwa hivyo, ni vizuri kuona kuwa tunawalea watu wetu katika hali nzuri ili waweze kujisaidia katika hali ya sawasawa.

Pia, nataka kusema kuwa mambo ya matibabu hayapendi siasa wala chukuchuku. Kwa hivyo, ni muhimu sana sisi wanasiasa tuwaunge mkono wataalamu ambao wanafanya kazi zao katika hospitali. Ni vizuri kuwatetea na kuangalia kile ambacho hawana katika hospitali ili tuwasaidie wawe nacho ndio waweze kutoa huduma bora kwa wananchi wetu wa Kenya. Kuna kelele nyingi siku hizi. Katika Kenyatta National Hospital kumetokea matatizo kama Mbunge mwenzangu, Mhe. Wanyonyi, alivyozungumzia. Leo matatizo yametokea na watu wanaruka wakitaka Waziri Sicily Kariuki aende nyumbani. Nataka kusema kitu kimoja kwa huyu waziri. Ana siku mbili au tatu alizokuwa katika afisi ile. Kwa hivyo, jambo la muhimu ni kuacha kuingilia mambo ambayo hatujakuwa na utaalumu zaidi. Tunamuunga mkono Waziri Sicily

Kariuki na tunataka afanye kazi yake bila kumingilia. Na penye matatizo tusi-*mvictimise* bali tuhakikishe kwamba amefanya kazi yake vizuri na hospitali hizo zimepata dawa na kuweza kuendelea kuwahudumia Wakenya.

Kwa hivyo, namuunga mkono ndugu yangu, Mhe. Mohamed Ali, Mbunge wa Nyali; kwa kuleta Hoja hii na kuona kuwa Hoja hii haitarudishwa nyuma. Kamati ya Utelekelezaji ifanye juhudi kuona kuwa yale tuliyoyafanya yametekelezwa. Serikali, kupitia Kamati ya Bajeti, ione kuwa pesa zimetengewa shughuli hii. Kando na kuwa na Hospitali ya Rufaa na Mafunzo ya Eldoret na hii ya hapa Nairobi, sisi watu wa Mombasa tungenda kujivunia kuwa na hospitali ya rufaa. Ninasema hivyo kwa maana gavana wangu, Mhe. Ali Hassan Joho amejizatiti katika Hospitali ya Coast General, Mombasa. Ameirekebisha na kuitengeneza lakini mpaka dakika hii, tukiangalia hospitali ile, haiwahudumii watu wa Mombasa peke yake. Inawahudumia watu kutoka sehemu tofauti tofauti. Kwa hivyo, Serikali inapaswa kutuma pesa ili tufungue hospitali ya rufaa na tusaaidiane na magavana wetu ili wananchi wetu wapate huduma bora ya afya.

Kwa hayo machache, namuunga mkono Mhe. Mohamed Ali, na kusema Wabunge wengine tuchangie na kuunga mkono Hoja hii ya matibabu.

The Temporary Deputy Speaker (Hon. (Ms.) Tuya): Sawa kabisa. Waheshimiwa, ningependa kuchukua fursa hii kuwatambua wanafunzi wa Kilabu cha Mijadala kutoka Chuo Kikuu cha Kirinyaga ambao wako kwenye ushoroba wa nyumba. Wanatoka Eneo Bunge la Kirinyaga ya Kati katika jimbo la Kirinyaga.

Tuwakaribishe.

(*Applause*)

Mhe. Chebet Tum.

Hon. (Dr.) Tum: Mhe. Naibu Spika wa Muda, nataka kuunga mkono Hoja hii iliyoletwa na Mhe. Ali. Tunajua kwamba Kipengele cha 25 cha Katiba ya Kenya na Kipengele cha kwanza cha Sheria ya Afya vinasema kwamba tutaweka hospitali ya rufaa katika kila jimbo. Nataka kusema kwamba watu wanakufa wengi sana kwa sababu hawana dawa na vifaa ambavyo vinafaa katika hospitali zetu. Hoja hii itawasaidia Wakenya sana. Sisi Wabunge tunaitwa kila wiki kushughulikia watu wengi ambao wako na shida. Tuko na magonjwa mengi kama ugonjwa wa saratani, ugonjwa wa figo na watu wameuza mashamba wakabaki hohehahe. Hawawezi kuwapeleka watoto wao shuleni kwa sababu wanalazimika kwenda kupata huduma kwenye hospitali za kibinafsi na kulipa Kshs4 milioni. Inabidi mtu auze shamba lake la ekari tano ili apatiwe dawa zinazofaa. Tunajua kwamba tuko na hospitali mbili za rufaa. Tuko na moja kule Eldoret na pia tuko na ile ya Kitaifa ya Kenyatta. Tunajua kwamba hospitali ya Mombasa inahudumia kaunti sita. Tumeona kuwa watu wa Mombasa wanataabika sana na tunaiunga mkono Hoja hii.

Tunajua kwamba kama kuna shida katika hospitali wanaoteseka ni kina mama. Kwa nini ninasema kina mama wanateseka? Kina mama wako na kazi nyingi kule nyumbani. Baba wa nyumba akiwa mgonjwa, mama wa nyumba huacha kila kitu kuhakikisha kwamba watoto wameenda shuleni. Tunajua kwamba katika hospitali zetu za kaunti hakuna dawa wala mitambo ya kuwashughulikia watu wanaougua ugonjwa wa figo. Hatuna mashine za kuwashughulikia watu wenye ugonjwa wa saratani. Tunaweka hii iwe *priority number one* katika nchi yetu ya Kenya.

Tunajua Serikali ya Jubilee iko na ajenda nne. Moja ya hizo ni kupatia kila mmoja matibabu ya kufaa. Tukitaka kuendeleza hii ajenda tuanzishe hospitali za rufaa katika kaunti

zote. Tangu tulipopata Uhuru mwaka wa 1963, tuliapa kwamba tutaangamiza matatizo ya ugonjwa, upumbavu na umaskini. Lakini umaskini unachangiwa na kutokuwa na hospitali za rufaa. Hali hiyo inasababisha watu kuuza ardhi yao ili waweze kupata huduma katika hospitali za kibinafsi. Hakuna Mbunge ambaye hali. Mimi kama mama kaunti wa Nandi ninaitiwa harambee ishirini kila mwishoni mwa wiki. Tunaomba Serikali itusaidie kwa sababu kupeana dawa na kila kitu ni kazi ya Serikali. Mshahara mdogo tunaolipwa hautoshi kisimamia harambee ya kuchangia watu. Hii ni kwa sababu ya magonjwa, kuchangia watoto wa shule na kila kitu. Utaona Mbunge akijiongelesha peke yake kwa sababu hawezi kupata pesa za kumchangia mtu aliyelazwa hospitali. Ninaomba tuweke maanani afya ya watu wetu. Tupitishie yale Mhe. Ali amesema. Na haitakuwa Mombasa peke yake, kwa sababu watu wetu wanakufa sana. Tuwe na hospitali za rufaa katika kila kaunti na tuweze kutimiza ajenda moja ya Serikali ya Jubilee.

Asante.

The Temporary Deputy Speaker (Hon. (Ms.) Tuya): Sawa kabisa msheshimiwa. Ningependa kuwakumbusha wahemishimiwa kwamba utakapoanza kwa lugha moja uweze kukamilisha mjadala wako na lugha hiyo. Tukumbuke kuingea na Mhe. Spika ili tutofautishe vikao vyetu hapa kutoka ile mikutano yetu ya hadhara katika maeneo ya Bunge.

Afuataye ni Mhe. Mwadime, Mbunge wa Mwatate.

The Temporary Deputy Speaker (Hon. (Ms.) Tuya): Samahani nimepoteza kadi yako hapa.

Hon. Mwadime: Shukrani, Mhe. Spika wa Muda, kwa kunipatia fursa hii. Asante sana. Umenitambua kwa sababu nilikuwa nimekuja mbele kabisa. Bahati mbaya mwenzangu kwa ile *shagala bagala* ukapitiwa ukashika kadi yangu kwa bega lake basi ikabanduka.

Kabla hata sijaongea, kwa kweli na dhiti kabisa, naunga mkono hii Hoja. Kabla sijasahau, najua wenzangu hapa wameongea kuhusa masuala ya maji. Nadhani katika awamu ya Bunge la 11, nilipitisha Hoja ya maji na Wabunge hapa waliunga mkono kwa wingi kabisa kuwa kila taasisi ya umma ipate maji. Hiyo Hoja ilipita vizuri lakini kwa sasa hivi mpaka dakika hii hatujui imefiki wapi. Nimejaribu kuifuatilia kila mahali lakini ninatupwa huku na kule. Kwa hivyo, Kamati Tekelezi ni vyema ifuatilie hiyo Hoja. Ikiwezekana maji ipatikane kila mahali ndiyo magonjwa mengi yapungue.

Kwa sasa hivi, mimi kama mwakilishaji wa Eneo Bunge la Mwatate naona saratani inatumaliza. Na ni kweli watu wengi sana wana saratani. Juzi tu, nilikuwa na Mbunge wa kwanza ambaye alikuwa anawakilisha Eneo Bunge la Mwatate. Alikuwa anateta na kuuliza kwa nini Bunge isifanye bidii ili kila kaunti angalau ipate mashine ya kuangalia saratani. Mwenzangu wa Nyali, Mhe. Ali, kwa kweli hii Hoja ameitunga na ikatungika. Tunasema tutaifuatilia ili itekelezwe. Kama vile Mbunge wa Jomvu alivyosema, tusikuwe na mambo ya mchezo maanake magonjwa kwa kweli hayataki siasa. Wakenya tutakuwa tumesaidika. Mwanzo tuanze na ile mikoa ya zamani nane. Kila mkoa angalau upate hospitali ya rufaa, na vile vile tuangazie kila kaunti.

The Temporary Deputy Speaker (Hon. (Ms.) Tuya): Samahani, tafadhalini Waheshimiwa. Ningependa kuomba hivi: Najua Hoja hii inachangamsha watu wote na inagusia hali ambayo ni tatanishi katika kila sehemu Bungeni. Ningeomba tafadhali nifuatilie mpangilio ambao nimeupata hapa, kwa sababu mkija wote kwangu hapa, mtanichanganya. Kwa hivyo, tufuate ile orodha ambayo iko hapa. Ningependa kusema kwamba tuko na wakati. Tunaenda mpaka saa saba. Ningeomba unaposimama kuchangia, jaribu kufupisha maneno yako ili tuweze kuwapatia wengine nafasi ya kuchangia.

Asante. Endelea msheshimiwa.

Hon. Mwandime: Mhe. Spika, nadhani kila Mbunge amesikia. Hii Hoja itasaidia Wakenya kwa ujumla maanake watu husafiri kutoka maeneo mbalimbali. Tukiangalia hali ya mfuko kwa kila mtu, kwa kweli haiendi sambamba. Kifungu 43 cha Katiba kinaambatana pia na kile cha ugatuzi. Kinasema kwamba ikiwezekana, hela izidi kusukumwa kwa wingi kule mashinani. Najua kuna changamoto maanake ugatuzi ulianza juzi. Wakipelekewa pesa kwa wingi, nafahamu kaunti zetu zitatatua hili tatizo la magonjwa.

Vile vile, kupata dawa limekuwa tatizo katika hospitali ya Serikali. Hii Hoja ikitekelezwa, najua itapunguza taabu kwa wingi. Kwa sababu wenzangu wameongea sana na nikiongea nitakuwa narejelea yale, natoa shukrani kwa kunipa hii fursa. Asante sana, Mhe. Spika wa Muda.

The Temporary Deputy Speaker (Hon. (Ms.) Tuya): Mhe. Rahim Dawood

Hon. Dawood: Nakushuru, Mhe. Spika wa Muda. Kwanza, ninampongeze ndugu yangu, Mhe. Mohamed Ali, kwa kuleta Hoja hii ya kuanzisha hospitali ya rufaa kule Mombasa. Nasikitika kwamba katika Bunge lililopita, tulipitisha Hoja nyingi. Hata mimi nilipitisha Hoja ya kuweka chumba cha wagonjwa mahututi katika kila kaunti, na hata kila eneo Bunge kwa Kenya nzima, lakini mpaka leo, Kamati ya Utekelezaji haijasema ni nini itafanyika. Hoja hili ambayo imeletwa na Mhe. Mohamed Ali ni nzuri hasa mambo ya kuanzisha hospitali ya rufaa Mombasa. Pia zikuwe kila pembe ya nchi yetu ndio tuweze kuangalia mambo ya ugonjwa.

Tuna changamoto kwani hatuna madaktari. Hata wakati nilikuwa nikileta Hoja yangu, tulikuwa tunasema hatuna madaktari. Mhe. Mohamed Ali ametuambia leo kwamba madaktari wanalipwa pesa kidogo. Lazima tufikirie ni kitu gani tutawafanyia madaktari wetu. Hatutakuwa na madaktari kila siku, wanaenda kwa hospitali kisha wakirejea nyumbani hawana pesa kwa mfuko. Wanafanya kazi kutoka asubuhi mpaka usiku na hata ukiwapigia saa nane ya usiku unatarajia wakuwe hospitalini, lakini hawana fedha. Tukiwa nchi na Wabunge, lazima tufikirie Kenya yetu inaenda vipi. Tunaelekea vizuri ama la? Kama hatuna afya kama Kenya nzima, basi hatutaendelea mbele.

Nashukuru, Mhe. Ali amesema tunaweza kujenga hospitali na Kshd3bilioni, na tuziboresha zile zilizoko ili ziwe hospitali za rufaa na Kshs2bilioni. Nauliza ni nani anatoa hizo pesa, kama sio Bunge kutenga hizo pesa ziende kwa hospitali?

Katika Kaunti yangu ya Meru, tulikuwa na hospitali ya Level 5. Kwa wakati huu, Gavana wetu, Hon. Kiraitu, anaipoleka ikuwe Level 6. Nasikitika miaka 15 iliyopita, tulikuwa na mashine ambazo zilitoka Spain lakini hatuna wataalamu wa kuzitumia. Katika Kenya yetu, lazima tutafute wataalamu ili mashine zilizoko kwa hospitali ziweze kutumika.

Nashukuru Serikali ya India kwa kutupatia mashine ya babatron mwaka uliopita ya kuangalia saratani. Lakini tujiulize kweli kama mashine moja ndiyo itafaa Kenya nzima ambayo ina idadi ya watu 45milioni. Serikali na Bunge, lazima tupitishie pesa zile na ziangaliwe zisikuwe na sakata ya ufisadi, kama zile za Afya House ambapo tunasikia Kshs5 bilioni zinapotea. Wale wamechukua hizo pesa lazima wachukuliwe hatua na tusiwadhulumu madaktari.

Wiki mbili ama tatu zilizopita, daktari katika Hospitali ya Kitaifa ya Kenyatta alifanya upasuaji mtu asiyefaa. Kama angekimya, nani angejua amefanya vibaya? Hakuna mtu angejua. Ni vizuri alisema amekosea. Sasa tusiwalaumu hao. Waziri Cecily Kariuki amesema hajafuta kazi yule Mkurugenzi Mkuu wa Hospitali ya Kitaifa ya Kenyatta, Ms. Lily Koros. Amesema akae kando ndio mambo yaangaliwe kwa sababu Hospitali ya Kitaifa ya Kenyatta ina shida nyingi. Lazima tuone tutakavyofanya. Lakini tukisema kwamba tutampeleka nyumbani kwa sababu ya kumfuta 'mtu wetu'... Kwani nani siyo mtu wetu? Kila mtu Kenya hii ni mtu wetu!

Kwa hivyo, lazima tujue kwamba ikiwa tunataka kuendesha Kenya lazima tuelewe kuwa sisi ni ndugu hata kama tunatoka makabila tofauti.

Ugonjwa haujui ndugu wala dada. Inatupasa kuwa na hospitali za rufaa Kenya nzima. Tutenge pesa kwa ajili ya hospitali za rufaa. Pia, tunapaswa tuhakikishe kuwa hospitali za rufaa zinasimamiwa na Serikali kuu wala siyo za gatuzi. Hii ni kwa sababu magavana hawawezi kutekeleza wajibu wa kuwalipa madaktari na wafanyakazi wengine.

Kwa hayo machache, naiunga mkono Hoja hii. Ni changamoto kwa Mhe. Ali afuatilie Hoja hii ili tuweze kupata hospitali hii. Tumeshapitisha Hoja kumi na moja humu Bungeni lakini mpaka leo... Mhe. Mwadime amesema kwamba Hoja yake ya maji haijapita na yangu ya hospitali ya *intensive care unit* (ICU) na *blood donor unit* sijaona ilhali tunahitaji vitu hivyo.

The Temporary Deputy Speaker (Hon. (Ms.) Tuya): Nampa nafasi Mhe. King'ara Ng'anga.

Hon. King'ara: Asante sana Naibu Spika wa Muda, kwa jicho lako la ujasiri kwa kuniona na kunipatia mwanya wa kuchangia mjadala huu ulio na uzito mkali, kama vile ulitangulia kusema pale mwanzo.

Kila mtu hapa ameguzwa kwa njia moja ama nyingine na masuala ya kiafya. Si mzaha kusikia joto kali kutokana na usemi wa kiongozi wetu kutoka Mombasa, "Jicho Pevu". Na ni jicho pevu halisi. Ni vizuri kutilia uzito mkuu masuala ya afya kuliko mambo mengine yoyote yale. Ni afya njema imetuwezesha kuja hapa na hata kutupatia nguvu ya kucheka.

Langu ni kuwakumbusha Wabunge na Wakenya kwa jumla kuwa Kenya iko na maeneo matatu makubwa: Nairobi, Mombasa na Kisumu. Eneo la Mombasa ni njia moja ya kuingia katika nchi yetu. Kuna njia tatu za usafiri: anga, ardhi na maji. Mombasa ndiyo eneo kubwa sana la kuingiza mizigo katika nchi yetu. Tumepata gari moshi la kasi hivi juzi. Ingekuwa bora ikiwa tungepata mambo mengine kwa mwendo wa haraka, kwa mfano mambo ya kudumisha afya njema. Kama vile mwenzangu amenena hapo mbeleni, Mombasa inaathiri maeneo mengi. Ni vizuri tuwe na hospitali kubwa ya rufaa katika eneo la kisiwa cha Mombasa.

Kuna wengine walichangia hapa kuwa katika vyuo vikuu hapa nchini, tunafunza madaktari wengi sana lakini wakimaliza masomo yao, hawafanyi kazi hapa kwetu. Ni vizuri sisi Wabunge tujiulize kwa nini watu wetu wanasoma na hawatuhudumii. Wengi wameenda kufanya kazi ughaibuni. Je, huko ughaibuni kuna nini ambacho hatuna hapa? Kwa nini sisi tukaachwa nyuma? Sisi Wabunge inastahili kutenga hela za kuziimarisha hospitali zetu. Na kama vile wengine wamesema, kama tumepata ugatuzi, kwa nini tusipate ugatuzi rasmi kwa mambo yote, hasa kiafya?

Nimetoka Ruiru, si Mombasa. Eneo langu liko na watu 600,000. Katika hospitali kuu hapo Ruiru, akina mama hujifungua watoto 26 kila siku. Hata leo watapatikana. Vitanda vya watoto ni 12. Vitanda vya wanaume ni saba peke yake. Je, hayo ni maendeleo kweli? Sharti turudi nyuma kidogo tuchunguze ni wapi tulipotea na kuacha kuzingatia masuala ya afya katika nchi yetu. Hakuna mtetezi wa wanyonge!

Asante sana ndugu yangu, Mhe. Mohamed Ali Mohamed, kwa kujitokeza kuwatetea wanyonge. Wale watu maskini waliotupatia kura tukajipata hapa Bungeni ndio wasioweza kujitetea. Wacha tuchukue fursa hii tuwatetee ndio wapate mwanya wa kuishi maisha mazuri kama sisi. Hiyo itapatikana tukiunga mkono mjadala huu kwa kishindo ili mambo mazuri yapatikane kwa hawa wanyonge.

Nilikuwa na hofu kidogo wakati tumekaa hapa Bungeni tukiongea kuhusu mijadala muhimu iliyo na maendeleo mwafaka katika nchi yetu. Kulikuwa na upinzani kidogo hapa. Hapa tumepata mwanya mzuri sana wa kufanya kazi kama kikundi kimoja. Kwa vile upande wa

Upinzani na sisi katika upande huu mwingine tunaongea kwa lugha moja kuhusu maendeleo, basi mimi naona hata hii hospitali itajengwa haraka hata kuliko anavyotarajia ndugu yangu. Hilo likifanyika, basi litakuwa limeambatana na zile ajenda nne zilizopendekezwa na kiongozi wetu wa Jubilee, Uhuru Kenyatta.

Sitasahau kuwakumbusha kwamba hata katika zile hospitali chache za rufaa tulizonazo, vifaa vya matibabu havipo. Ndiyo maana unaona watu wengi bado wanaenda ng'ambo. Hata kama tutachangia na kujenga hospitali za rufaa, itabidi sisi Wabunge tutenge fedha zitakazotumiwa katika utafiti wa magonjwa hasa yale yanayotuathiri. Kenya ni nchi ambayo imeendelea kama mnavyoyua. Sijui ni nini twakosa hata tukashindwa kujimudu kimaisha hasa kiafya? Kama mnavyoyua, Wakenya wote wanatuangalia sisi Wabunge wao. Kwa hivyo, si King'ara hapa peke yake - Hata wewe, pahali popote pale uwakilishapo, mwananchi anakuangalia na afya yake iko mikononi mwako. Hii ni kwa sababu wewe ndiwe umehitimu kuwatetea na kuleta mijadala kama hii ambayo itawapatia afya njema kule mashinani na mijini.

Sitasema mengi kwa vile nataka kuwapa muda wengine ambao wamekuwa wakingojea tangu asubuhi kama mimi. Naunga mkono Hoja hii na kushukuru sana kwa vile upande wa Upinzani umetuunga mkono kufanya kazi pamoja kama Wakenya.

The Temporary Deputy Speaker (Hon. (Ms.) Tuya): Sawa kabisa. Nampa nafasi Mbunge wa Jimbo la Migori, Ochieng Awuor.

Hon. (Ms.) Ochieng: Thank you, Hon. Temporary Deputy Speaker. Much as we are speaking Kiswahili today, I have waited until the spirit of speaking Kiswahili is gone. So, I will try it tomorrow.

I stand to support this Motion by my good friend "Jicho Pevu". The truth of the matter is that the issue of health in Kenya is a painful one to think about. This idea of having several referral hospitals in various parts of our country is overdue, especially at the county levels, at least to start with. All of us are harassed because people are sick and dying. When we go to the counties and constituencies, the communication is one, namely, death and sickness. Like in the case of cancer, quite a number of our women are dying of cancer, especially cancer of the uterus and the breast. We all know that as the medics say, they can be helped if there are equipment and facilities that can detect this kind of diseases in good time. I fully support this Motion.

Look at the case of Migori County. We have a Level 4 hospital which has nothing. Any small thing, including just a chest x-ray, you would need to take a patient to Kisii. That would take you a whole day or two because the doctor to interpret the x-ray is not there. Any other case more serious than that has to be brought all the way to Tenwek, which is quite a distance. Most of those people live below the poverty level. Even getting funds for transport to bring them to those far-flung hospitals is a big issue. It is our humble appeal that putting everything else aside, the national Government and the devolved government need to give the issue of health priority so as to save the lives of our people. When we have a healthy population, the community can work to reduce poverty and other ills that affect the society.

Hon. Temporary Deputy Speaker, the other major reason why we need to have these hospitals at county levels, as much as we appreciate the existence of Kenyatta National Hospital and, indeed, it has done a good job over the years, is that it has come to pass that some of the facilities they have are outdated and doctors are few. They are overwhelmed because every other person, from Wajir to Mandera and from other parts of the country go to Kenyatta National Hospital for treatment. When you go there, you witness a pathetic scenario. No wonder we are having issues like a sick person who was not supposed to undergo brain surgery being operated on by mistake. It shows that there is something wrong and that these people are overwhelmed. It

is high time we created other facilities to ease congestion and make those in charge of the hospitals operate under bearable circumstances. We need to look at children's health. I want to reiterate that all over this country, the number of orphans we have is increasing by the day.

Sometimes patients from some parts of the country are too sick to go to Kenyatta National Hospital or Moi Teaching and Referral Hospital on their own. So, another problem is created. The person coming all the way from Ntimaru, for example, to come to take care of the patient in Kenyatta National Hospital has no place to live or a has nothing to eat. These are some of the issues we should consider. If we can have referral hospitals near where such people are and facilities are provided such that people can be taken care of near where they live, we will do this country a very good service. We may not need to over-emphasise this. Our people need to be healthy, need to be treated and need to have access to good medical facilities. This is a matter of life and should be given priority. Everyone has a right to life.

I support this Motion fully. I wish as we pass it, as one speaker said, we should not just pass the Motion, but a special budget should be put aside to make sure that as we move on in the next five years, each county in Kenya should have a good referral hospital that can take care of people.

Because much has been said, I do not have to over-emphasise this. On behalf of women and on behalf of the marginalised, I support this Motion that we get a good referral hospital in Mombasa, Migori, Kakamega, Busia and all other counties for the welfare of our people.

Thank you very much.

The Temporary Deputy Speaker (Hon. (Ms.) Tuya): Hon. David Sankok.

Hon. ole Sankok: Asante sana, Mhe. Naibu Spika wa Muda. Kiswahili ni lugha letu la taifa na ni lazima tujivunie kama Wakenya. *Hon. Temporary Deputy Speaker, protect me from ...*

The Temporary Deputy Speaker (Hon. (Ms.) Tuya): Mhe. utahitajika kuamua kama utaongea kwa lugha ya Kiswahili kutoka mwanzo hadi tamati ama ukiamua utatumia lugha ya Kimombo, utamalizia kwa lugha hiyo.

Hon. ole Sankok: Asante sana, Mhe. Naibu Spika wa Muda.

Hon. Ali Sharif: Hoja ya nidhamu, Mhe. Naibu Spika wa Muda.

The Temporary Deputy Speaker (Hon. (Ms.) Tuya): Mhe. Ali, ni jambo gani lisilo la kinidhamu?

Hon. Ali Sharif: Asante sana Mhe. Naibu Spika wa Muda. Kwa kuwa Kiswahili ni lugha ya kitaifa, naomba kisitumike kwa njia isiyo. Ni makosa kutumia lugha ya Kiswahili kwa namna ambayo sivyo na kuiharibu. Asante.

(Laughter)

The Temporary Deputy Speaker (Hon. (Ms.) Tuya): Tutampatia kila mtu nafasi ya kujieleza. Hata lugha ya Kimombo hukanganya watu wengi. Kwa hivyo jambo muhimu ni tuelewe vile Mhe. ananena lakini abaki katika laini ya lugha moja.

Hon. ole Sankok: Asante sana, Naibu Spika wa Muda. Mhe. anatoka eneo la Pwani na Kiswahili chake ni cha kiwango cha cha juu kidogo. Lakini tutajikakamua tukinene. Leo tutaongea Kiswahili.

Naunga mkono Hoja hii ambayo imewasilishwa na Mhe. Ali, ambaye pia tunamjua kama "Jicho Pevu". Hoja hii ambayo ameleta Bungeni tutaiunga mkono kama Wabunge na pia Wakenya wote. Hoja yenyewe inazungumzia shida ambayo imekuwa ikitukabili kama nchi. Ni shida ya afya yetu. Kama nchi, hatuwezi kuchezea afya yetu. Ni lazima tuhakikishe kuwa fedha

za kutosha zimetengwa ili isiwe Hoja zinaletwa Bungeni na baada ya kuzijadili, na kuafikiana kama Wabunge, zinakufia hapa; baada ya miezi ama miaka kadhaa hatuoni yale tumepitisha kama Wabunge.

Hongera Mhe. Ali. Hili ni tatizo kubwa sana. Kenya nzima ina hospitali mbili peke yake za rufaa ambazo ziko mbali kutoka nyingine. Watu kutoka Pwani huja hadi Hospitali ya Kitaifa ya Kenyatta. Inawachukua muda na watu wetu wanaaga njiani wakati wanasafirishwa. Hii ni shida kubwa sana. Hoja ya Mhe. Ali inafaa itiliwe maanani kabisa ili tuwe na hospitali ya rufaa Pwani. Lakini isiwe Pwani peke yake. Upande wa Kaskazini mwa Kenya pia inahitaji hospitali ya rufaa kwa sababu ni mbali. Watu wa eneo hilo hawawezi kusafiri kuenda Eldoret kwa urahisi. Ni mbali pia kwao kuja Nairobi. Hata tukiwa na Hospitali ya rufaa huko Pwani, itakuwa mbali kwa watu wa kaskazini mwa Kenya.

Tuko na shida pia ya migomo ya madaktari. Hawagomi bure. Madaktari sio kama wafanyikazi wengine wa Serikali. Wanafanya kazi masaa 24. Wanaitwa usiku wa manane, kwa mfano, kushughulikia mgonjwa ambaye labda walimtibu mchana lakini hakupata nafuu na anataka kuonana na daktari aliyemtibu wakati wa mchana. Inabidi daktari huyo amke ili aende kazini. Tunapoteza madaktari kwa sababu nchi jirani wanalipa madaktari vizuri kuliko Kenya. Kwa hivyo, inatajikana pia tufikirie tutambue shida yetu. Tunatoa mafunzo kwa madaktari wengi katika vyuo vikuu. Siku hizi, Chuo Kikuu cha Kenyatta na kile cha Kilimo na Teknolojia cha Jomo Kenyatta vimeanzisha mafunzo ya udaktari. Pia tuko na wauguzi wanaosomea vyuo vya mafunzo ya uuguzi. Lakini ukitembelea hospitali zetu za Serikali, unapata hao madaktari hawafanyi kazi huko. Wengi wao wamefungua hospitali za kibinafsi kwa sababu ladba wanapata pesa. Wengine wamehamia nchi za kigeni. Inabidi tuhakikishe madaktari wanahudumu kwa hospitali zetu za serikali.

Watu wote hawana uwezo wa kuenda kwenye hospitali za kibinafsi kwa sababu ya gharama ya juu. Ni uchungu sana ukiona mama akibeba mtoto afikishe kwa hospitali lakini daktari hawezi kumsaidia kwa sababu hana dawa. Ikiwa kuna vifaa ambavyo havipatikani kwenye hiyo hospitali, daktari anamtuma huyo mama anunue hivyo vifaa ama dawa kwenye maduka ya madawa lakini huyo mama hana uwezo. Daktari anaangaliana na mama mpaka mtoto anakufa mkononi mwa mama kwa sababu ya ukosefu wa vifaa katika hospitali zetu. Ni uchungu mkubwa. Sisi ambao tunatunga sheria tuko na uwezo wa kupelekwa ng'ambo tunapokua wagonjwa. Tumeona watu ambao wamepelekwa ng'ambo kuwekwa bandeji pekee wakigongwa kidogo na mawe. Kuna wenzetu ambao wanakufa kwa ugonjwa ambao unatibika. Katika karne hii, ugonjwa wa malaria unaua watu humu nchini licha ya kwamba tuko na aina zote za dawa za malaria. Unakuta ugonjwa wa pneumonia unaua watoto nchini Kenya ilhali tuna dawa za kukabiliana na magonjwa kama hayo. Kwa vile madawa hayo hayapatikani kwa urahisi katika hospitali za umma, matibabu yanakuwa ni kwa watu walio na pesa. Kulingana na Kifungu 43 cha Katiba yetu, afya bora ni haki ya kila Mkenya. Siku hizi afya bora ni haki ya walio na pesa, na siyo haki kwa wasio na pesa. Ni lazima tulitilie maanani na tulizingatie suala zima la afya.

Ninataka pia kumwambia Mhe. Ali kuwa tukishaipitisha Hoja hii, afuatilie kuona kuwa imetekelezwa. Ikibidi urudi Bungeni ili tuweze kutoa maagizo, afanye hivyo ndiyo masuala yanayoshughulikiwa na Hoja hii yasiishie hapa Bungeni. Hii itatuwezesha kuhakikisha maombi yote tunayoyapitisha hapa Bungeni yametekelezwa ili Wakenya wote waweze kupata matibabu.

Hata kama nimeongea Kiswahili ambacho kidogo kinatatiza, ninajua kwamba nimejikakamua. Mhe. Omollo, ahsante kwa kuja kutuunga mkono. Umemaliza kazi yako. Sasa nitakuwa nikipambambana na nani? Sasa kazi yangu imeisha. Hiyo handshake imemaliza kazi yangu.

The Temporary Deputy Speaker (Hon. (Ms.) Tuya): Mhe. Baya Yaa, Kilifi North.

Hon. Baya: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika wa Muda kwa kunipatia nafasi hii. Nimesimama kuunga mkono Hoja ambayo imeletwa na ndugu yangu Ali ambaye anatoka eneo la Pwani.

Hospitali ya rufaa ya kiwango cha sita huko Pwani imechelewa kufika. Mimi ningependa kuongea kwasababu hospitali hii ya Mombasa iwekwe kama hospitali ya rufaa. Kwanza, kuna magonjwa mengi hapa duniani ambayo huathiri watu wanaoishi Pwani. Ni magonjwa ambayo hayawezi kufanyiwa utafiti katika maeneo mengine. Matibabu yake yanafanyika vizuri yakifanyiwa pale Pwani. Saa hii pale Mombasa, kuna ugonjwa wa Chikungunya, ambao unaathiri wapwani peke yao.

Kuna magonjwa mengine kama vile tende guu ambayo yako katika eneo la Pwani peke yake, na matibabu yake hayawezi kupatikana mahali pengine popote humu nchini. Kwa hivyo, kama tunataka kuwasaidia watu wa Pwani na kuhakikisha kwamba wamepata haki yao ya kikatiba, kulingana na Kipengee 43 cha Katiba, ni haki kwamba hospitali ya Mombasa ifanye hospitali ya rufaa.

Pili, hospitali ya Mombasa imekuwa pale muda mrefu kabla hospitali nyingine hazijajengwa humu mchini. Pengine Hospitali Kuu ya Kenyatta peke yake ndiyo inatoshana na hospitali ya Mombasa ki-umri. Hospitali ile imesahaulika licha ya kwamba ni hospitali ambayo wakati wa ukoloni na baada ya kupata Uhuru ilitiliwa maanani sana. Hospitali hiyo ilikuwa ikopewa kila kitu lakini ikafika wakati ikaachiliwa. Sasa, tuko na wakati mwafaka kwa sababu ya kile ndugu yangu Sankok alichokitaja kuwa handshake. Sasa tunataka ile handshake pia ifike kule Pwani ili tuone matunda yake. Tunataka ile hospitali ya Mombasa iwe tunda la kwanza la ile handshake. Sisi Wapwani tutafurahi. Pengine ningefanya ukarabati wa hii Hoja kusema kwamba haya mambo yawekwe katika Bajeti ya mwaka huu wa kifedha ili tuhakikishe kwamba hospitali ya rufaa ya Mombasa inatimilika.

Tatu, hospitali ile inasaidia kaunti karibu nane za Kibwezi, Lamu, Tana River, Taita Taveta, Kilifi na maeneo mengine. Watu wote huteremka Mombasa kutafuta matibabu. Zaidi ya watu milioni kumi nchini huenda kwenye hospitali ile kutafuta matibabu lakini ukiangalia ambulensi ambazo zinaenda Mombasa, zote huelekea kwenye hospitali za kibinafsi, ambazo zina gharama kubwa kwa watu wetu.

Jambo lingine ambalo ningependa kusema ni kwamba kuna ugonjwa wa saratani ambao umekithiri zaidi Mombasa na sehemu ya Pwani kwa jumla, kwa sababu ya madini mazito ama heavy metals yanayopatikana katika eneo lile. Utafiti unaonyesha kwamba watu wengi katika Kaunti ya Kwale wameathirika kutokana na ugonjwa wa saratani. Katika kaunti ya Kilifi, kwa sababu ya kuweko kwa madini mazito aina ya iron ore na titanium, ambayo yako na carbon, wakazi wanaathirika kutokana na ugonjwa wa saratani kwa urahisi kuliko wakazi katika sehemu zingine za Kenya. Kwa sababu hiyo, na kwa sababu ya uchafuzi wa hewa unaofanyika Mombasa, tunahitaji usaidizi wa haraka ili hospitali ya Mombasa iweze kupandishwa cheo na kuwa hospitali ya rufaa.

Nikimalizia, kwa sasa kuna utafiti ambao unafanywa. Pale kwetu kilifi, kuna kitengo kinaitwa Kenya Medical Research Institute (KEMRI) ambacho kinafanya utafiti wa tropical diseases. Ule utafiti kwa sasa umeonyesha kuwa watu wengi wa Pwani wanaathirika na tropical diseases ambazo matibabu yake hayapatikani humu nchini. Tukifanya hospitali ya Mombasa kuwa ya rufaa na kuweka vyombo ambavyo vitatuwezesha kupata matibabu ya magonjwa hayo, itakuwa tumefanya jambo la busara. Kwa sasa, kuna vyuo vikuu viwili kule Pwani ambavyo vinajaribu kutoa mafunzo ya udaktari – Chuo Kikuu cha Pwani kilichoko pale Kilifi na Chuo

Kikuu Cha Teknolojia cha Mombasa. Hivyo vyuo vimeshindwa kutoa mafunzo ya matibabu kwa sababu hakuna hospitali ya rufaa na mafunzo. Kama tunataka kuvikuza vyuo hivyo ili viwe taasisi za elimu zinazoheshimika, ni lazima tuhakikishe kwamba mafunzo ya udaktari hayapatikani Nairobi peke yake, bali yanapatikana katika vyuo hivyo pia. Kwa hivyo, tuna wajibu wa kuhakikisha kwa haraka sana kwamba hospitali ya Mombasa imefanywa hospitali ya rufaa na mafunzo kama hospitali za Edoret na Kenyatta.

Ni matumaini yangu makubwa kwamba Hoja hii itatiliwa maanani na Serikali. Kabla sijasahau, miongoni mwa maono manne makubwa ambayo Rais Uhuru Kenyatta ametangaza ni matibabu bora kwa kila Mkenya. Ndiyo tuweze kuyafikia malengo hayo, inatubidi sisi Wakenya na Serikali kuhakikisha kwamba hospitali za rufaa pia zimepewa kipaumbele. Rais hawezi kutimiliza ile ndoto ya universal healthcare ambayo iko kwa ile Big Four Agenda yake; hawezi kuafikisha haya maono yake kama ile hospitali ya Mombasa itabakia vile na zile hospitali ndogo ndogo pia zitabakia vile. Ni matumaini yangu hospitali ya Mombasa ikukuzwa kuwa ya rufaa, zile hospitali ndogo ndogo katika Mkoa wa Pwani zitafanya mabadiliko makubwa katika kuhakikisha kwamba watu wa Pwani na Kenya wanapata matibabu yanayofaa ambayo Serikali inatumainia kuyapata.

The Temporary Deputy Speaker (Hon. (Ms.) Tuya): Mheshimiwa mwakilishi wa eneo la Mosop, Tuwei.

Hon. Tuwei: Asante sana Mhe. Spika, kwa lugha ya Kiswahili “Kinara” kwa kunipa nafasi pia, nichangie katika wazo hili ambalo ni la muhimu sana kwa watu wetu na nchi yetu kwa jumla. Hongera mwenzangu, mheshimiwa Jicho Pevu kwa wazo ambalo umelifikiria na kufanya utafiti ambao umeuchukulia kimaanani kwa kutoa maelezo ambayo ni ya kweli.

Jambo ambalo ningependa kushukuru ni kwamba tuko na hospitali mbili za rufaa hapa nchini ambazo ni Kenyatta na Eldoret. Lakini, hospitali hizi ziko na shida: wagonjwa ambao wanaletwa pale ni wengi zaidi ya uwezo wa hospitali hizo. Kwa mfano, Hospitali ya Mafunzo na Rufaa ya Moi – Eldoret imekuwa hospital ya pekee; inapokea wagonjwa kutoka sehemu zote, hata kutoka nchi jirani yetu za Uganda, Sudan, Somalia na sehemu zote ambazo zinakaribiana kwa sababu tuko na uwanja wa ndege pale. Jambo ambalo ni nzito ni idadi ya wagonjwa wanaoletwa pale ambao wangepaswa kutibiwa na mahospitali yaliyo karibu. Kwa hivyo, hospitali yenyewe imekosa ule umuhimu wake wa kuwa hospitali ya rufaa. Imekuwa hospitali ya kutibu magonjwa madogo madogo ambayo yangepasa kutibiwa na hospitali zile zingine za kaunti, za Kiwango cha 3 au 2 kule nyuma.

Ya pili ni kwamba tuko na tatizo katika jamii kwamba mtu anakuwa mgonjwa zaidi, ikifika kiwango fulani anakimbizwa pale wakati imekuwa kero. Sisi pia kama wananchi tuko na shida. Sisi viongozi ambao tuko hapa tunajua ya kwamba kila wikendi, kila kuchao, sisi ndio tunaitwa kwa michango na matibabu. Nashukuru kwamba afya kwa wote imezingatiwa katika yale mawazo manne ya Rais. Naona itatusaidia zaidi iwapo sisi sote kama vingozi tutaweza kupitisha Mswada na pesa ambazo zitatekeleza wajibu huu wa kupea wananchi wetu afya bora.

Cha muhimu ni kwamba ni kweli kwamba tuko na madaktari. Ni kweli kwamba tunaongoza katika eneo hili la Afrika Mashariki kwa upande wa matibabu. Cha muhimu ni kwamba usimamizi wa hospitali zetu na viongozi ambao wameteuliwa kama Mawaziri na makatibu kusimamia kiungo hiki hawajawajibika. Kuna hofu kuhusu dawa ambazo zinaletwa nchini. Madaktari husema kuwa dawa nyingine ambazo zinatumika hazipitii barabara nzuri kwa udhibiti; inachangia wazo la kuongezea magonjwa mengine kama saratani kwa sababu dawa zinaozolingia humu nchini hazipitii utaratibu unaofaa. Inafaa wakati tunaenda kuyapitisha

mambo haya tuyachunguze na kuona ya kwamba kila kitu ambacho tunala kiwe kimepitishwa katika mpangilio ambao utatuepusha na magonjwa.

Vile mheshimiwa mwenzangu amesema hapa, maji tunayotumia yana madini ambayo yanasababisha magonjwa mengine. Hili ni jambo ambalo lazima tuliangalie, kama viongozi na nchi.

La nne ni kwamba lazima tujiulize tunataka nini kama viongozi. Kila kiongozi anayekuwa Rais angependa kuwacha mambo fulani ambayo atakumbukwa kwayo. Namshukuru mstaafu Rais Moi kwa sababu wazo hili la kuweka Hospitali ya Mafunzo na Rufaa ya Moi mjini Eldoret ni lake wakati wake ule. Tunamshukuru sana. Mungu amusaidie apate ubora wa afya anapozeeka. Hii ni ili sisi sote tujue kwamba ni muhimu tupitishhe Hoja hii kwa haraka. Ni jambo ambalo limefanyika jana kwamba hata yeye mwenyewe mstaafu Rais amepelekwa kule atibiwe na hali tuko na uwezo, tumesoma na tuko na rasilimali ambazo tunaweza kutumia kuyakuza mambo haya.

Ya mwisho ni kwamba, tulivyo kama nchi, wananchi wakiwa wagonjwa ama wageni wetu wanapozuru nchi, cha muhimu wanachoangalia ni: “Je, nikienda nchi ya Kenya, nipate matatizo ya matibabu, nitapata hospitali ambayo inaweza kunitibu?” Lazima tuwe watu wanapanga mambo yao mbele ili tupate kuimarisha utalii na vile, tupunguze gharama ambazo nchi hii inapitia kwa kuwapeleka wagonjwa wetu nje kwa matibabu.

Naunga mkono wazo la kusema kwamba wale wanasimamia hospitali zetu, haswa za saratani, wapeane nafasi kwa nchi nyingine zijenge hospitali hapa; hospitali ambazo zitakuwa nafuu kwetu kwa kutumia teknolojia yao. Nchi ya India iko na matibabu ya gharama ya chini na ya njia bora kuliko nchi zingine ulimwenguni kama Marekani na Ulaya.

Nikifunga, hospitali hizi mbili ambazo tunasema ni za rufaa haziko katika kiwango kimoja. Kuna tofauti kubwa sana kati ya mishahara ya wafanyakazi wa Kenyatta wa na rufaa ya Eldoret. Daktari wa Kenyatta National Hospital na daktari wa Hospitali ya Mafunzo na Rufaa ya Moi kule Eldoret wana tofauti ya mishahara ya Kshs100,000 na zote ni hospitali za rufaa. Kama hospitali hizi mbili ni za rufaa, lazima mishahara yao isawazishwe kwa sababu inachangia madaktari kutoka kwa hospitali moja kwenda kwa nyingine. Msimamizi wa Kenyatta anashinda msimamizi wa Hospitali ya Mafunzo na Rufaa ya Moi ya Eldoret kwa zaidi ya Kshs200,000 kwa mishahara. Hilo ni jambo la kushangaza sana. Juzi Waziri wa Hazina ya Taifa ambaye anatakiwa kuangalia jambo hili anakalia sana pesa za kupeana huduma za hospitali hizi. Utakuta kwamba hata huduma ya kutolewa kwa hospitali hizi zina shida. Ukiangalia bajeti ya KNH na ya Hospitali ya Mafunzo na Rufaa ya Moi – Eldoret, kuna shida kubwa sana.

Ni ombi langu kwa Wizara ya Fedha kuwa pesa za hospitali zitolewe kwa haraka bila kuchelewa ili kupunguza shida ambazo tunapata. Kwa hayo machache, nashukuru.

The Temporary Deputy Speaker (Hon. (Ms.) Tuya): Mbunge wa Eneo la Gilgil, Mhe. Wanjira.

Hon. (Ms.) Wanjira: Ahsante sana, Naibu Spika wa Muda. Ningependa kuchukua nafasi hii kumpongeza Mhe. Mohamed Ali kutoka Eneo Bunge la Nyali kwa kuleta Hoja hii Bungeni. Mengi yamesemwa na sitayarudia, lakini la muhimu sana ni kutimiza Malengo Endelevu ya Maendeleo yanayojulikana sana kama SDGs. Ikiwa hatuwezi kuwapatia wananchi wetu afya njema, basi hatutakuwa tunazingatia malengo hayo. Ukikadiria kuwa watu milioni 44 wanategemea hospitali mbili peke yake za rufaa nchini, utaona kuwa tuna shida. Kwa Mhe. Ali, ningependa kusema, hata ingawa umeileta kama Hoja, usikome hapo kwasababu nilipokuwa Seneti katika Bunge la 11 tulipitisha Hoja nyingi sana na kutekeleza Hoja hizo ambazo si sheria ilikuwa vigumu zaidi. Usikome hapo; leta Mswada tuupitishhe katika Bunge hili ili tuwe na

sheria ambayo itatengewa pesa kwenye Bajeti. Isiwe tu ni kusema na kunena bila kutekeleza. Azimio lilitolewa kule Abuja mwaka wa 2001. Tusiseme tu tuweke viwango fulani vya hospitali ila tuzungumzie uzuri wa hospitali katika kila kiwango. Aidha tuhakikishe pesa zinazowekwa kwenye Bajeti zinalingana na kila kiwango. Nasema hivyo kwa sababu, kwenye Azimio la Abuja, ilisemekana kuwa kiwango cha chini sana cha pesa kiwe ni 15% kwenye Bajeti nzima. Kama nchi bado tuko mbali, lazima tujikakamue kuafikia lengo hilo. Ingawa maeneo mengine ya ugatuzi yamejaribu, hatujafikia kiwango hicho.

Hospitali ambazo zimeorodheshwa kama Kiwango 5 ni 12 tu nchini. Ziko Nyeri, Thika, Nakuru, Mombasa, Meru, Kisii na Embu. Walipozigawa, ilikuwa zisambazwe katika maeneo yote nchini. Tusiongeze tu kiwango cha hospitali bila kuongeza madaktari, vifaa vinavyohitajika na pesa kwenye Bajeti. Tunaweza kuanzia mahali ikiwa hizi hospitali 12 tutazifanya kuwa za rufaa. Hospitali ya rufaa lazima iwe hospitali ya rufaa. Hivyo ni kusema yale magonjwa madogo yatibiwe katika zahanati na hospitali za viwango vya kaunti ama kaunti ndogo. Kwa mfano, ile hospitali ya Nakuru PGH ambayo ni kiwango cha tano, iwahudumie watu kutoka maeneo tofauti lakini siyo wagonjwa wa malaria, upangaji wa uzazi, ama homa na mafua. Wagonjwa aina hiyo wapelekwe katika zahanati. Siyo eti ukitaka kupanga uzazi, ama ukitaka dawa za wanaoishi na virusi vya ukimwi unaenda hospitali ya rufaa ya Kenyatta. Dawa hizi zinafaa zipatikane kwenye zahanati. Kwa hivyo, lazima wahudumu wawe waadilifu.

Nasema hivi kwa sababu ingawa tunaenda kutimiza hili Lengo Endelevu la Maendeleo la Tatu ama SDG 3 ama ajenda mojawapo ya serikali ya Jubilee, waliopewa kazi kwenye maeneo tofauti nchini... Tumeona kwenye magazeti kuwa kuna ufisadi katika utekelezaji wa bima ya NHIF. Kuna shida ya ufisadi wa mamilioni ya pesa. Wakati kuna shida kama hiyo, hatuwezi tukafikia lengo hili. Kuna wakati mtekelezaji mkuu aliachishwa kazi. Madaktari wengi walipopatiwa hiyo kazi walisema hawaitaki kwa sababu inahusishwa na ufisadi kwenye hospitali hiyo. Waliogopa kupakwa tope. Lazima kila mtu akipewa kazi awajibike.

Ningependa pia kusema kwamba kama kuna watu ambao wameumia sana kutokana na shida hizi ambazo kila mtu anaongelea ni akina mama na watoto. Ni mwaka wa 2018 na bado tunaongea juu ya vifo vya akina mama zaidi ya elfu kumi ambao hufariki wakati wanajifungua. Ni aibu kubwa kwa taifa. Kama tutaanza na hospitali 12 zilizoko kwenye maeneo tofauti tofauti, tutakuwa tumepiga hatua kubwa. Baadaye, tutaimarisha hospitali kuu katika kila gatuzi nchini. Kwa hayo machache, naunga mkono na kumpongeza tena Mhe. Mohamed Ali kwa Hoja hii.

The Temporary Deputy Speaker (Hon. (Ms.) Tuyu): Mhe. Mwakilishi wa Mwingi North.

Hon. Nzengu: Shukrani sana Naibu Spika wa Muda, kwa kunipa nafasi hii niweze kuchangia mjadala huu. Kwanza ningependa kumshukuru Mhe. Mohamed Ali kwa kuleta Hoja hii ambayo inamgusa kila mtu. Tukiongea maneno ya siha ama afya, ni jambo linalomlenga kila mwananchi wa Kenya. Sitaki kurudia maneno yaliyosemwa na Wabunge wenzangu, lakini kabla sijachangia sana, ningependa kumkosoa Mhe. King'ara aliyesema Rais Kenyatta ni Rais wa Jubilee. Rais Kenyatta ni Rais wa Kenya na chama cha Jubilee ndicho kilichompeleka mbele akawa Rais. Maneno ya chama sasa yameisha na sisi tuliokua upande huu tumekaribiana sasa. Watu wa Jubilee mjue sasa Rais ni wa Kenya.

Nikirudia Hoja iliyoko mbele yetu, ningependa nikubaliane na Mhe. Ali ila nitapendekeza marekebisha machache. Kwa mfano, nitataka arekebishe Hoja kwa kusema, 'Hospitali ya Mombasa ya Rufaa na Mafunzo' kwa sababu kuna vyuo vikuu Mombasa ambavyo vinasomesha mafunzo ya afya. Juzi tuliona madaktari wakifanya makosa kwa kumpasua kichwa

mtu ambaye hakufaa kupasuliwa. Lazima pia tutilie mkazo masomo ya afya. Haiwezekani kuwepo mafunzo ya afya bila kuwepo maabara na hospitali za mafunzo.

Nakubaliana na Hoja hii kwa sababu gharama ya kuwapeleka wagonjwa nje ya nchi kama vile India, Tel Aviv... Tunayo habari kwamba aliyekuwa Rais wetu yuko Tel Aviv. Hivi juzi kiongozi wa chama chetu cha Wiper alikuwa ujerumani akakaa kule kwa miezi kadhaa. Tunajua kwamba ni wengi wetu ambao wamekuwa wakienda nchi za nje kutafuta matibabu. Naomba tutengeneze hospitali zetu za rufaa hata kama watalaamu hatuna wengi, tuwalete kutoka nchi za nje, tuwakodeshe kwa miezi au miaka kama tulivyokodesha vifaa vya kutibia ugonjwa wa saratani. Labda ule muda uliyoopanwa wa kukodi vifaa vile ufupishwe na ukiisha tuangalie namna ya kununua vifaa vyetu. Hii ni kwa sababu nimeelezwa kwamba hata vifaa vidogo vidogo kama makasi sharti tuvinunue sasa. Kwa hivyo, ningependa turekebishe namna ya kukodesha vifaa vya kutibu saratani.

La mwisho, nimeiskia kutoka kwa wale Wabunge waliokuwa Bunge la 11 kuwa kuna Hoja na sheria nyingi zilipitishwa kama vile Mhe. Mwadime na Mbunge wa Meru walivyosema. Naibu Spika wa Muda, ningependa kama inawezekana uitishe hiyo Miswada ama Hoja ili tuchukue likizo ama nafasi tuzizungumzie na tuipe ile kamati tekelezi jukumu hilo.

Mwisho kabisa, ningependa kuwashukuru wanafunzi wa Shule ya Upili ya Kamuwongo ambao wametembelea Bunge hili leo. Ni shule katika eneo langu la Bunge. Hao ni viongozi wa kesho watakaokuwa Wabunge kama mimi.

Asante sana, Naibu Spika wa Muda.

The Temporary Deputy Speaker (Hon. (Ms.) Tuya): Mhe. Ali Athman, tafadhali unaweza sasa kutetea lugha.

Hon. Ali Sharif: Asante sana Naibu Spika wa Muda kwa kunipa nafasi hii ili niweze kuchangia mjadala huu muhimu ambao unaangazia masuala ya afya ya Wakenya.

The Temporary Deputy Speaker (Hon. (Ms.) Tuya): Samahani Mhe. Ali. Ningependa kuwapa fursa wale wanaotaka kuchangia mjadala huu na ningependa kumuomba mwenye Hoja awape dakika moja wale ambao hatutaweza kuwafikia kwa sababu wakati wa kufunga unapokaribia. Mhe. unaweza kuendelea na mjadala wako.

Hon. Ali Sharif: Naibu Spika wa Muda, kabla ya kuendelea, nilikuwa nimeomba hoja ya nidhamu kuhusiana na suala hili nzima. Hoja hii inaonekana imetia hamasa wengi na wangependa kuchangia lakini naona muda haupo nasi maana umetupa kisogo. Pengine kupitia utaratibu wa Bunge hili, Sheria za Bunge, Kifungu Nambari 97(4), ningependa muda wa kuongea pengine upunguzwe kutoka dakika kumi hadi tano ili wenzetu wengine nao waweze kupata fursa ya kuchangia ikiwa itawezekana.

Naibu Spika wa Muda, ningependa kumpongeza Mhe. Ali kwa fikira ya kuleta Hoja hii hapa. Vile vile, ningependa kumpongeza kwa ule utafiti ameweza kufanya kikamilifu kuhusiana na suala nzima la afya katika nchi yetu ya Kenya. Pengine kadri tunavyoendelea kujadili suala hili ndivyo tutakapoweza kuuliza tatizo liko wapi na limesababishwa na nini. Hii ni kwa sababu, linaonekana kama kwamba katika karne hii ambayo tuko, wengi wanaochangia swala hili hawajaridhishwa na huduma ya afya nchini Kenya. Vile vile, tunajua kuwa ni pesa nyingi ambazo zinatumiwa katika nyanja hii ya afya hususan baada ya Wakenya kusema kuwa huduma hizi zipelekwe mashinani na zigatuliwe.

Ningependa kushukuru wale wahusika mashinani ambao wameweza kushughulikia suala hili kwa namna ambavyo wameweza kufanya. Lakini, tatizo hili bado lipo na wakenya wengi wanateseka. Sio kwamba pengine nitazungumzia eneo Bunge langu la mashinani bali hata Nairobi kuna watu wanaoishi humu lakini wakishikwa na homa hawajui waende wapi ama

watasaidika namna gani. Kama nilivyosema, kuna umuhimu wa kuangalia suala hili na kuliangazia kwa undani kabisa. Tatizo ni nini na limesababishwa na nini?

Naibu Spika wa Muda, Hospitali ya Mombasa kwa hivi sasa hakuna asiyejua kwamba inapokea wageni kupitia kila sehemu katika masuala ya matibabu. Iwe ni wageni kutoka Lamu, Kilifi ama sehemu tofauti, wote huenda Hospitali ya Mombasa. La kusikitisha ni kuwa Bunge hili likikaa kugawanya pesa za mashinani ama za kaunti ama kugawanya pesa katika Bajeti yake kila mwaka, sijaona mambo haya yakifikiriwa.

Jambo ambalo ningependekeza tunaposubiri ujenzi ambao umependekezwa wa hospitali nyingine kule Mombasa, tayari hospitali hii inahudumia na kupeana huduma ambayo tuko nayo. Tatizo tu ni kwamba huduma hizi haziwezionekana kukamilika ikiwa Bajeti ya nchi hii haiweki kisawasawa na kusema kwamba kwa sababu fulani tumepea hospitali ya Mombasa bajeti ya ziada ili iweze kujimudu na mambo kama haya huku tukipanga namna jinsi tutakavyojenga hospitali nyingine ya Level 6. Kadri tunavyoendelea kuishi katika nchi hii, tukumbuke pia kwamba idadi ya watu inaongezeka. Idadi ya watu ikiongezeka kuna dharura ya mambo yanayoweza kupanuliwa ili yaongezeke.

Naibu Spika wa Muda, suala lingine lililojadiliwa ni suala la madaktari. Mhe. Ali amepena idadi ya madaktari walioko Kenya. Pengine, tujiulize ni kwa nini madaktari ni wachache hivyo. Pia, ni kwa nini hao madaktari hawana imani ya kufanya kazi Kenya hii. Hayo ndiyo mambo tunayotaka kuyajua ili tuyatafutie suluhisho. Madaktari wengi wanaosomea taaluma hii huenda kufanya kazi nchi za nje kwa sababu malipo huku ni duni. Kwa hivyo, suala la malipo kwa madaktari ni kitu muhimu sana kitakachofanya madaktari wawe na imani na utulivu wa kufanya kazi hapa Kenya. Vile vile, inawagharimu pesa nyingi sana wale wanaosomea udaktari. Hivyo basi, ningependa Serikali iwe na mipangilio maalum ya kuwasomesha takriban vijana 500 wanaotaka kusomea taaluma hii ili idadi ya madaktari iongezeke kadri idadi ya watu inavyoongezeka.

Naibu Spika wa Muda, matatizo ni mengi. Kuna haja ya kuhakikisha mwananchi wa kawaida amepata huduma hizi. Ingawaje Serikali bado inajitahidi, bado kuna tatizo. Tatizo kubwa lipo katika wahusika wakuu ambao wanaendeleza mambo haya. Kama viongozi, tunafaa kusimama kidete na kuyaweka mambo kama haya sawasawa. Mambo mengi huzungumzwa hapa lakini ukienda mashinani hakuna hata moja limeweza kufanyika. Kuna dharura ya Wakenya kusaidika kiafya kwa sababu rasilimali ya kiumbe chochote ni afya. Sisi kama binadamu tunafikiria pengine rasilimali zetu kubwa ni masuala ya pesa lakini jambo muhimu sana ni afya ya binadamu. Tunahitaji kuizingatia pakubwa na kuhakikisha tumefuatilia haya na yamekuwa sawa kwa wale wenzetu wanyonge, vile ilivyozungumzwa kuhusu wale hawawezi kujimudu kupata matibabu ya gharama za juu.

Naibu Spika wa Muda, kuna watu ambao hawajielewi katika nchi hii. Mtu anaamka asubui na hajui atajisaidia namna gani na familia yake huku tayari kuna uzito wa magonjwa na kadhalika. Kwa hivyo, kama nchi pia tujaribu kuangalia uchumi wa watu wetu ili kuwasaidia kupambana na mambo kama hayo ya magonjwa yanapofika.

Ningependa kuunga mkono na ningependa Bunge hili liwe pamoja ili kupitisha Hoja hii. Tuweze kufuatilia jambo hili na kuhakikisha kwamba Mkenya wa kawaida anasaidika na haya tunayozungumzia hapa.

Asante.

The Temporary Deputy Speaker (Hon. (Ms.) Tuya): Sawa kabisa, Mhe. Athman. Ningetaka kutoa mwongozo kidogo.

Mheshimiwa, ulisema ya kwamba ingekuwa bora kama tungepunguza muda wa kujadili Hoja hii lakini kulingana na muongozo wa mipangilio ya Bunge, muko na uwezo kama waheshimiwa. Wewe Mhe. Athman si Mbunge mpya. Hata hivyo, unaweza kuwasilisha Hoja hiyo kabla hatujaanza mjadala wa ile Hoja nyingine. Nafikiri tunaalewana. Kwa hivyo, tukiwa na mjadala wowote ambao unachangamsha watu wengi na wengi wanataka kuuchangia, tuna njia ya kuweza kupunguza wakati lakini kabla ya Hoja kuanza. Nitachukua fursa hii kuwatambua na kuwakaribisha wanafunzi kutoka Shule ya Upili ya Wasichana ya Manunga, kutoka Eneo Bunge la Kipipiri katika Jimbo la Nyanadrua. Tuwakaribishe.

(Laughter)

Tumsikize Mhe. Njiru Muchangi kutoka Eneo Bunge la Runyenjes.

Hon. Eric Njiru: Thank you so much, Hon. Temporary Deputy Speaker for giving me an opportunity to add my voice to this good Motion. I also thank the Member for Nyali, Hon. Mohammed Ali, for this very good Motion. I thank him for his very fluent Kiswahili that has inspired so many other Members to speak in Kiswahili.

Healthcare is a very important issue in this country. I am certain that if we were given an opportunity to choose between being healthy and being wealthy, all of us would choose to be healthy. The reason as to why so many Kenyans are flocking private and mission hospitals is because of the very poor services that we sometimes receive in our public hospitals. Therefore, we end up going to Kenyatta National Hospital, which is a referral hospital, to seek services that we would have gotten in other hospitals and health centres. I wish to support the idea of having a Level 6 Hospital in Mombasa County but at the same time applaud the efforts being made by the Government of Kenya, in partnership with universities such as Kenyatta University. We are aware that there is a teaching and referral hospital that is almost about to be opened at Kenyatta University. We believe that this and more would help Kenyans access healthcare in this country.

I wish to bring to the attention of this House some statistics with regard to the access to the National Hospital Insurance Fund (NHIF). The NHIF is a programme meant to help so many Kenyans access healthcare. The statistics that we have show that only around six million Kenyans are covered by NHIF. Out of those, only around four million are consistent in paying the premiums. Where are the rest? We have around 15 million Kenyans who are not covered by NHIF and so they cannot access basic healthcare in many hospitals. Why are they not covered? We are aware that Kenyans in formal employment who earn a monthly salary of about Kshs6,000 and below are required to pay Kshs150 per month for their NHIF insurance. Those of us who earn Kshs100,000 and more are supposed to pay Kshs1,700 for their NHIF medical insurance.

Every other person is classified as “self-employed” and is required to pay Kshs500 per month for NHIF medical insurance. The reality is that so many Kenyans are not able to pay Kshs500 per month for healthcare because we have many Kenyans who live in abject poverty. Therefore, as we discuss the issue of opening up many regions to better and greater healthcare, it is important that this campaign is aligned with Jubilee’s Big Four agenda for Kenya. It is good for us to look at the NHIF issue so that we make it more affordable for Kenyans.

As I conclude, it is important for us leaders not to politicise healthcare. As we speak, we are all aware that we have leaders who are pursuing the impeachment of one Cecily Kariuki, who is the Cabinet Secretary for Health. It is also common knowledge that Kenyatta National Hospital in the last one month has been in the news for the wrong reasons. So, we are saying that

two weeks is not good enough time to determine or gauge the performance of a CS. Therefore, those pursuing her impeachment should abandon that move and allow her perform her duties and rescue the many Kenyans who are seeking services at KNH.

Those of us who have had time to go to that hospital can agree with me that we have many people who have been at that hospital for many months, but who have not got the services they are looking for. Therefore, it is good that we do not politicise this matter so that we do not bring to a halt the services that Kenyans are looking for at our hospitals.

With those few remarks, I support the Motion.

The Temporary Deputy Speaker (Hon. (Ms.) Tuya): Mhe. Hassan Maalim, nitakupa dakika mbili, halafu nitampa dakika mbili Mwakilishi wa Jimbo la Mombasa.

Hon. Hassan Omar: Thank you, Hon. Temporary Deputy Speaker. I have been here quite early and have been looking forward to this opportunity.

At the outset, I wish to say that Mohammed Ali has done the right thing in bringing this Motion to the House. Healthcare in Kenya needs a serious radical surgery in all aspects in terms of infrastructural development, human resourcing and financial support. This must be done not only in Mombasa. Specialised healthcare is required in all the counties, and especially in far-flung counties like Mandera where I come from. The issue of concern in Mandera is that it has the highest maternal mortality rate in the world. This has been so because of lack of specialised doctors and equipment for various ailments.

Mombasa is the hub for the coastal region, starting from Tana River County to the North and Taita Taveta County to the West. It is surprising that Kenya does not have a specialised hospital in that region, which has a population that is growing fast. I therefore support the Motion and request the national Government to put more resources into the health sector so that the lives of Kenyans can improve.

Thank you.

Hon. (Ms.) Asha Mohamed: Asante sana, Mhe. Naibu Spika wa Muda. Naunga mkono Hoja ya kiongozi mwenzangu, Mbunge wa Nyali, Mohamed Ali, kama mama kiongozi wa Mombasa Kaunti.

Hospitali kuu ya Pwani ambayo iko Mombasa Kaunti inahudumia mkoa wa Pwani na kutoa huduma ya afya. Kwa hivyo, Hoja hii ya ndugu yangu Mohamed in muhimu ili tuweze kujenga hospitali ya rufaa na kuhakisha kwamba itapatiwa kipaumbele ili pia iwe na chuo kikuu. Hivi juzi nimerudi kutoka Ujerumani ambako nilipata matibabu mazuri sana katika Chuo Kikuu cha Ujerumani. Kwa hivyo, tukiweza kupatia hospitali zetu fedha na kuziinua katika kiwango kinachofaa ili wananchi wapate huduma, itakuwa vizuri. Zaidi, huko Hospitali kuu ya Pwani na pia zahanati zingine kuna shida kubwa ya linda mama. Ningependa tuhakikishe kwamba linda mama inafwatiliwa haraka ili akina mama waweze kupata huduma zaidi katika zahanati zote huko Mombasa na Kenya kwa jumla.

Asante sana, Mhe. Naibu Spika wa Muda.

The Temporary Deputy Speaker (Hon. (Ms.) Tuya): Sawa Kabisa. Waheshimiwa, tumetamatisha Hoja. Ninampatia mtoa hoja nafasi hii ili aweze kuhitimisha. Unaweza kuwa mkarimu na kuwapatia Waheshimiwa wenzako dakika moja ya kuchangia.

Hon. Mohamed Ali: Asante sana, Mhe. Naibu Spika wa Muda. Naona mjadala huu unazidi kuwaka moto na Wabunge wanachangia vilivyo. Hata hivyo, kabla sijahitimisha Hoja hii nitakuwa mkarimu na kuwapa Wabunge wafuatao dakika moja: Mhe. Mwashako, Mwololo, Jeremy, Nakara na Mbunge wa Nyando. Mhe. Abdullswamad, Mbunge wa Mvita kwa sababu

yeye ni jirani wangu na ndiye mwenye hospitali hii ambayo tunaipigania iweze kuboreshwa zaidi, nitampa dakika mbili.

Shukrani.

Hon. Mwakuwona: Asante sana, Mhe. Naibu Spika wa Muda. Kwa kweli, mjadala huu ni mzito. Hoja iliyoletwa na ndugu yangu Mhe. Mohamed Ali wa Nyali naipongeza. Nimepata kuchangia kwa dakika moja lakini ningetamani kuichangia kwa muda wa kutosha. Nilikuwa nimejiandaa vilivyo kuzungumza mambo mengi, lakini, nitataja mawili tu ya muhimu.

Kwanza, tunapoangazia hospitali iliyoko Mombasa ni vizuri tutathmini kwamba miaka iliyotangulia hadi Hoja hii imefika Bungeni leo, watu wamekuwa wakitoka kilomita zaidi ya mia sita ama saba kukimbilia hospitali ya rufaa hapa Nairobi. Sana sana wenzetu wanaotoka Tana River, Lamu, Taita, Kwale na Kilifi. Hii imekuwa ni changamoto kubwa. La msingi, watu wetu wanakimbilia sana Hospitali ya Pwani na mara nyingi haina vifaa vinavyofanya kazi. Tunapotathmini swala hili, tujue kwamba wananchi kutoka kaunti yangu ya Taita Taveta huenda Tanzania kutafuta matibabu. Juzi tumepoteza mama kule Tanzania ambae alifia huko na angekuwa amepata matibabu humu---

The Temporary Deputy Speaker (Hon. (Ms.) Tuya): Endelea Mheshimiwa.

Hon. Lomorukai: Asante sana, Mhe. Naibu Spika wa Muda. Kwanza, nigeponda kumpongeza mwenye Hoja kwa kunipatia dakika moja kwa sababu sikuweza kuchangia Hoja hii.

The Temporary Deputy Speaker (Hon. (Ms.) Tuya): Samahani. Huyu ni Mhe. Lomorukai Ekamais kwa sababu ya HANSARD.

Hon. Lomorukai: Asante sana. Kwanza, ningependa kumpongeza Mhe. Ali kwa sababu Hoja yake ni nzuri. Hoja hii itafanya sisi wengine ambao tunatoka sehemu za kaskazini magharibi mwa Kenya pia tunufaike kwa kupata hospitali ya Level 6. Itakuwa vizuri kama Hoja hii, baada ya kupitishwa, ifuatiliwe ili ifanye kazi mara moja.

Kuna sehemu zilipata hospitali za viwango vingine kama Level 4 au Level 5 na hazijawahi kupatiwa huduma nzuri. Kuziorodhesha hospitali hizo katika viwango hivyo haikuweza kuzisaidia. Muda wangu umeisha.

Ahsante.

The Temporary Deputy Speaker (Hon. (Ms.) Tuya): Mheshimiwa mwingine ni Mbunge wa Nyando. Mhe. Okelo Odoyo.

Hon. Okelo: Hon. Temporary Deputy Speaker, a referral hospital in Mombasa is a matter that is long overdue but even as we look at matters health, we have to give a holistic approach. We need Level 5 hospitals in all our counties to ease the pressure that is put on Kenyatta National Hospital and Moi Teaching and Referral Hospital in Eldoret. Again, I would also propose that we have referral hospitals in all our regions – the former provinces – so that our people can easily access healthcare. We have had our doctors incensed by the low pay but I think we also, as a Government, have to remunerate our doctors in a way that is pleasing to them so that we do not lose them as a result of brain drain to other nations.

Universal medical healthcare, which is done by NHIF, should be stepped up but I would propose that even as we do so, let us increase the number of physicians sitting on the NHIF board. Finally, the money that is meant to be transferred to counties as money following functions should be 80 per cent as opposed to the 20 per cent.

The Temporary Deputy Speaker (Hon. (Ms.) Tuya): Next!

Hon. Nakara: Ahsante sana, Mhe. Naibu Spika wa Muda. Ningependa kumshukuru rafiki yangu, Mhe. Ali kwa kunipatia nafasi. Hata tukiweka hospitali mbili au tatu za rufaa bado

tutakuwa na matatizo. Ili tuwajibike sawasawa na Katiba yetu ya Kenya katika Kipengele cha 43, njia mwafaka ya kumpatia mwananchi matibabu mazuri; kwanza, kuajiri wataalamu wazuri katika kila zahanati; pili, kuweka dawa katika kila zahanati; na tatu, kujenga hospitali za kiwango cha nne katika kila kaunti ili ziwahudumie watu wa chini. Hii ni kwa sababu hospitali za kiwango cha kitaifa hazitahudumia kila mtu.

Ahsante, Mhe. Naibu Spika wa Muda.

The Temporary Deputy Speaker (Hon. (Ms.) Tuya): Sawa kabisa. Mhe. Nassir.

Hon. Nassir: Ahsante, Mhe. Naibu Spika wa Muda. Ahsante ndugu yangu, Mhe. Mohamed Ali. Nataka kulikumbusha Bunge hili kuwa katika Bunge lililopita kuna Mswada nilioleta kubadilisha sheria na kuifanya Coast General Hospital ijulikane kama Pwani Referral Hospital. Nataka kutoa sababu. Wengi wametaja kuwa hospitali kuu zenye kusimamiwa na serikali ni mbili. La, si mbili. Ni nne. Ya kwanza ni Hospitali ya Kitaifa ya Kenyatta yenye wafanyakazi 6,000 na vitanda 800 lakini mpaka watu 3,000 wanaweza kulala katika hospitali hiyo. Ya pili ni Hospitali ya Rufaa na Mafunzo ya Moi ambayo ilipandishwa ngazi mwaka 2010. Wakati inafanyiwa *census*, wafanyakazi wake walikuwa 3,066.

Nataka kutoa hesabu. Katika hesabu ya fedha ya Bajeti ya mwaka 2014/2015, Hospitali ya Kitaifa ya Kenyatta ilipewa Ksh6.5 bilioni. Mwaka wa 2015/2016 ilipatiwa Ksh6.6 bilioni. Katika mwaka wa 2014/2015, Hospitali ya Rufaa na Mafunzo ya Moi ilipewa Ksh4.3 bilioni na mwaka wa 2016/2017 ikapewa Ksh 4.7 bilioni. Mathare Hospitali ni hospitali ya watu wenye akili punguani. Hospitali ya mwisho ilijengwa wakati wa ukoloni mwaka wa 1945. National Spinal Injury Hospital ina vitanda 25 pekee. Kwa hivyo, sio hospitali mbili mbali ni nne ambazo Serikali kuu inaweza kuangalia.

Baada ya kuweka Hoja hii, Mhe. Spika wa Muda, niliitwa na kongamano la magavana wa Kenya nzima. Walikuwa na mkutano wao pale Mombasa. Walielezea wazi ya kuwa hawana furaha na hili jambo la---

The Temporary Deputy Speaker (Hon. (Ms.) Tuya): Mhe. Ali, una dakika tatu lakini kama uko na ukarimu wa kuendelea kupeana nafasi kwa Wabunge wengine, unaweza kufanya hivyo.

Hon. Mohamed Ali: Shukrani sana, Mhe. Spika wa Muda. Labda kwa kuhitimisha katika Hoja hii ya siku ya leo ambayo imechangiwa vilivyo, kwanza kabisa nawashukuru Wabunge wenzangu walioweza kuchangia na wale wote ambao walikuwa wanataka kuchangia lakini muda haukuwaruhusu.

Ningependa pia kuwaambia kuwa Hoja hii ni ya taifa. Asilimia 80 ya Wakenya wana matatizo ya afya. Hoja hii bila shaka itakapofaulu na kufanywa sheria, itaweza kuhakikisha ya kwamba kila kaunti nchini Kenya imepata hospitali ya Level 6 ama hospitali ya rufaa.

Tumeweza kutoa takwimu mbalimbali na kuonyesha ni kwa nini tunahitaji hospitali hizi. Rais Uhuru Kenyatta mapema mwaka jana alisema ya kwamba anatoa pendekezo la kujengwa kwa hospitali katika kila kaunti. Kwa wale ambao waliingia wakati ambapo nilikuwa nikiendelea ama walichelewa kuingia, niliwapatia mifano mbalimbali na kuwaambia ya kwamba sisi tunaenda kinyume na Shirika la Afya Duniani (WHO). Shirika hilo linasema kuwa daktari mmoja anapaswa kuwashughulikia wagonjwa 1000. Hapa Kenya daktari mmoja anawashughulikia wagonjwa 10,000. Watu wanaumia sana. Tunazidi kumaliza kizazi. Tunazidi kuhakikisha ya kwamba watu wetu wanazidi kuumia badala ya kuwawakilisha katika Bunge. Tunawawakilisha katika mambo mengine yasiyo na maana. Naomba Bunge hili liweze kupitisha Hoja hii na kujua ya kwamba tuko tayari kukataa kuongeza majeneza Kenya ili tupunguze mzigo huu.

Ningependa kuwapongeza akina mama Wabunge wenzangu ambao mara kwa mara nawaona kwenye runinga wakati ambapo mama amepigwa katika visa vya nyumbani ama amebakwa, wanakimbia katika Hospitali ya Kitaifa ya Kenyatta kusimama naye. Leo nawataka msisimame nyuma ya mama huyo lakini msimame nyuma ya hospitali ili huyo mama asipate shida kutolewa Wajir mpaka Nairobi mbali apate huduma hizo hapo. Kwa hivyo, naona muda ndio huo umefikia kikomo. Langu nikusema tu asanteni sana na natumai idadi ya madaktari itaongezeka na hospitali zitajengwa.

Kwa Wabunge wote, nasema asanteni sana na Mungu awabariki.
Shukrani, Mhe. Spika wa Muda.

(Applause)

ADJOURNMENT

The Temporary Deputy Speaker (Hon. (Ms.) Tuya): Hon. Members, for obvious reasons, we will not put the Question on this Motion until such a time when it is put back on the Order Paper.

The time now being 1.03 p.m, this House stands adjourned until this afternoon at 2.30 p.m.

The House rose at 1.03 p.m.